Ecolebooks.com

JOSPA RELEASE VOLUME 1

© 2013

KISWAHILI KARATASI 2

102/2

(UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMU JAMII)

Karatasi 10 + Mwongozo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA I

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Watoto wamekuwa wakiteswa na kusumbuliwa sana kwa miaka mingi. Wengi wao wamekuwa wakinyimwa chakula, kukosa elimu, kuishi katika maisha ya dhiki na kufanyizwa kazi ngumu.

Lakini hapana msiba wa milele. Hali hii imeanza kubadilika baada ya ulimwengu mzima kutambua umuhimu wa haki za watoto.

Takriban mataifa yote ya ulimwengu ambayo ni wanachama wa umoja wa mataifa isipokuwa Somalia (ambayo haina serikali kuu) na Marekani yametiana saini makubaliano kuhusu haki za watoto. Makubaliano hayo yalifikiwa katika mkutano mkuu wa Umoja wa mataifa uliofanyika mwaka wa 1989. Hata hivyo, utekelezaji wenyewe wa makubaliano hayo ulianza mwezi wa Septemba mwaka wa 1990. Je, haki hizo za watoto ni zipi lakini? Haki za watoto zinaweza kupangwa katika makundi manne makuu ambayo ni: haki za kukua, haki za kuishi, haki za kulindwa na haki za kushiriki.

Haki ya kimsingi kabisa ni ile ya kuishi. Mtoto yeyote hawezi kufurahia haki zozote zile asipokuwepo, lazima awe hai. Maisha ya mtoto hayapaswi kukatizwa na chochote kile. Lazima ziwepo juhudi za kupinga vitendo vyovyote vinavyotishia maisha ya mtoto. Aidha, lazima mtoto atunzwe ipasavyo kimatibabu.

Haki nyingine ya watoto ni ile ya kulindwa. Aghalabu ulinzi wa mtoto hufanyika katika familia. Lakini sio watoto wote ambao wana bahati ya kuwa na familia inayoweza kuwapa ulinzi ufaao. Hawa wanapaswa kulindwa na kutunzwa na familia nyingine au na taasisi ambazo zinahusika na watoto. Ulinzi huo lazima ufungamane na sheria na utamaduni wa mtoto anayehusika. Mtoto pia ana haki ya kulindwa dhidi ya ajira ya watoto ambayo inawahusu watoto wanaofanya kazi wakiwa na umri wa chini ya miaka kumi na sita. Kazi huathiri ukuaji wa akili, kimwili, kijamii na hata kimaadili kwa mtoto anayehusika. Isitoshe, lazima mtoto alindwe dhidi ya mateso, dhuluma, adhabu na kunyimwa haki na uhuru wa aina

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

yoyote ile. Kwa mfano, haifai mtoto kuadhibiwa kwa hukumu ya maisha au kif'ungo cha maisha gerezani. Mtoto anapaswa kulindwa pia dhidi ya kubaguliwa kwa misingi yoyote ile, majanga, kulazimishwa kushiriki vitani na kuteswa kwa sababu ya maumbile yake. Pia tunapaswa kuhakikisha kuwa mtoto hateswi wala kudhulumiwa kwa sababu ya utamaduni fulani. Kwa mfano, zipo tamaduni zinazowalazimisha watoto wa kike kuolewa mapema au hata kupashwa tohara.

Haki nyingine kwa mtoto ni haki za maendeleo. Msingi mkubwa wa maendeleo ni elimu. Mtoto aliyepata elimu bora anaweza kuzielewa na kuzifurahia haki nyinginezo kwa njia nzuri na akawa anaishi maisha mazuri. Suala hili la maendeleo lazima lihusiane pia na uhuru wa kuweza kutambuliwa na kupewa utambulisho bila kubaguliwa.

Mwisho kabisa kuna haki ya kuishi. Haitoshi tu kuweza kuishi bali pia lazima mambo mengine muhimu yazingatiwe. Kwa mfano mtoto ana haki ya kupata habari kuhusu mambo mbalimbali yanayomhusu na kuhusu jamii yake. Habari ni msingi mkubwa wa kuwa na uwezo wa kujielewa. Mtoto anaweza kupata habari hizi kwa njia mbalimbali kama kupitia vyombo vya habari, kwa kupitia kompyuta n.k. Hata hivyo lazima mtoto huyo alindwe na picha au habari zinazoweza kumpotosha. Mtoto pia anao uhuru wa kushiriki na kujumuika na wenzake na hata kujiunga na vikundi vingine anavyopendelea. Haki hii ya kuishi haikamiliki bila ya kuwapo kwa haki ya kufikiri na kutoa maoni na hata kafanya maamuzi.

Jamii yetu inapaswa kushirikiana bega kwa bega kuhakikisha kuwa watoto hawatendewi dhuluma ya aina yoyote. Asilimia kubwa ya jamii zetu ni vijana ambao ndio tegemeo la jamii ya kesho. Ikiwa tunataka kuujenga msingi imara na mzuri wa jamii hiyo ya kesho, pana umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kuwa tumewatunza watoto vizuri.

Maswali:

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

1. i). Toa anwani itakayofaa sana kwa taarifa hii.. (Alama 2)

ii). Kifungu. "hapana msiba wa milele" ina maana gani kulingana na taarifa hii?(Alama 2)

iii). Je, ajira ya watoto ni nini? (Alama 2)

iv). Ajira ya watoto huwaathiri vipi? (Alama 2)

v). Maendeleo ya mtoto hayawezi kunawiri bila uhuru. Thibitisha (Alama 2)

vi). Mtoto atasaidiwa na nini ili aweze kupanua akili yake vizuri? (Alama 2).

vii) Msingi mkubwa wa maendeleo katika taarifa hii ni nini ? (Alama 1)

viii) Eleza maana za

2. -Takribani (Alama 1)

3. - Tia Saini (Alama 1)

2. **SEHEMU YA B: Ufupisho**

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo.

Uhalifu ni tendo lolote linalokwenda kinyume na matarajio ya watu, jamii, au taifa na linaloweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo ambao unakwenda kinyume na sheria za kidini au kanuni za kimaadili. Kwa mfano, mwananchi anayemwona mwenzake akiibiwa mkoba wake na kusimama bila kufanya lolote, amefanya kosa la kimaadili. Lakini tuangalie ni matendo yapi ambayo yanachukiliwa kama yanayokwenda kinyume na sheria za nchi, yaani matendo ya kihalifu?

Kuna matendo ya kihalifu yanayotendwa dhidi ya usalama wa umma au maadili ya jamii. Uhalifu dhidi ya mtu mwingine unahusu kitendo kinachomwathiri mtu mwingine kama mauaji, ubakaji na unajisi, wizi na ushambulizi. Uhalifu dhidi ya mali ambapo hapana uhusiano kati ya mtu mmoja na mwingine, huhusisha wizi wa kuvunja nyumba, uchomaji magari, uchomaji moto mali, wizi, na uharibifu wa mali. Uhalifu unaohusisha usalama wa umma na maadili unahusisha matendo kama uchezaji kamari, ukahaba,

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

uvunjaji wa sheria zinazohusiana na matumizi ya dawa, udanganyifu unaohusisha amana au mali ya umma na ulevi.

Uhalifu pia huweza kuainishwa kwa kutegemea adhabu anayopewa mhalifu anayehusika. Kuna makosa makubwa au makosa ya jinai na makosa madogo kisheria. Makosa ya jinai ni yale ambayo yanahusisha kifungo gerezani aghalabu cha zaidi ya mwaka mmoja. Kwa mfano, wizi wa kutumia nguvu, uporaji wa magari, mauaji na ubakaji ni makosa ya jinai.

Swali:

Kwa maneno yasiyozidi themanini, fupisha hoja kuu katika aya mbili za mwisho.

(Alama 15)

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

4. a) **Kanusha sentensi zifuatazo;** (alama 2)

(i) Uliugua malaria

(ii) Nimejenga kasri

b) **Andika nomino mbili katika ngeli ya U – YA.** (alama 2)

c) **Andika nomino zinazoweza kuundwa kutokana na vitenzi vifuatavyo.**(alama 2)

(i) Safiri

ii) Penda.

5. d) **Andika kwa umoja** (alama 2)

i) Machaka ya waridi hayazai maua meusi

ii) Walituandikia nyaraka ndefu.

e) **Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kila kivumishi cha pekee ulichopewa.**

(alama 2)

i) -Ote

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ii) –o-ote

f) **Onyesha vihisishi katika sentensi zifuatazo.** (alama 2)

i) Sawa sawa tutakutana kesho.

ii) Nabii Musa! Eti kifaru hula nyama

6. g) **Geuza sentensi zifuatazo katika <u>usemi wa taarifa</u>** (alama 4)

i) "Mabasi hayapiti hapa siku hizi, kuna nini" Mazrui aliuliza

ii) Karen: Tafadhali usiukanyage mguu wangu

Kadzo: Ah! Mbona niukanyage?

7. **Ukitumia mifano mwafaka, tunga sentensi kudhihirisha matumizi mbalimbali ya;** (alama 2)

i) Jinsi

ii) Ikiwa

8. i) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maelezo. (alama 2)

i) Mchwa wamezila mbao zetu zote. (Anza na mbao)

ii) Sijali hata kama hunipendi. (Andika kinyume)

j) **Kamilisha jedwali hili** (alama 4)

Kitenzi	Kutenda	Kutendana
Fa	…….	……
Cha	……..	……...

9. **Ukitumia <u>mchoro wa matawi</u>, onyesha <u>muundo wa sentensi</u> ifuatayo.**(alama 4)

Mtoto huyu alikunywa maziwa mengi

10. **Tofautisha maana za sentensi hizi.** (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

i) Ningalipandishwa madaraka, ningalinunua gari

ii) Ningepandishwa madaraka ningenunua gari

11. **Eleza matumizi ya ni katika sentensi hizi.** (alama 2)

i) Njooni kwangu nyinyi nyote

ii) Duniani waja wote ni sawa

n) **Taja aina ya vitenzi vilivyopigiwa mstari chini katika sentensi zifuatazo.**

12. (alama 2)

i) Huyu ndiye aliyetukomboa.

ii) Baba amekuwa mgonjwa

13. II. a) **Eleza maana ya semi zifuatazo** (alama 2)

i) Kata bei

ii) Tia ngoa

14. b) **Kamilisha majina haya ya makundi.** (alama 2)

i) Mkungu wa ……..

ii) Thurea ya ……

c) **Andika visawe vya;** (Alama 2)

i) Sarafu ……..

ii) Daktari …….

4. **ISIMUJAMII**

15. **(a) Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata** (alama 10)

A: Habari yako ndugu

B: Ndugu…… Ahh! (Anamsogelea) Bwana asifiwe!

A: Asifiwe sana ndugu!

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

B: Amen! Ahh ndugu yangu, imekuwa vipi umepotea hivyo?

A: Usiwe ha hofu ndugu. Nilikuwa nimeenda kuhubiri huko Nakuru. (Anatua kidogo). Ilinibidi niende huko, ili kutimiza amri ya Bwana.

B: Eeh, hata Yohana alienda kuhubiri ……

A: Habari ya siku nyingi?

B: Nzuri, Bwana ameendelea kunineemeshea baraka zake

A: Amen!

B: Nimeona mkono wake katika kila jambo

A: Amen! Asifiwe Bwana

B: Amen

A: Ameendelea kunibariki sana. Shetani hana nafasi katika maisha yangu

B: Shetani ashindwe

A: Ashindwe Ibilisi.

Maswali

16. i) Toa muktadha wa mazungumzo haya. (alama 1)

ii) Taja sifa zozote mbili zilizojitokeza katika mazungumzo haya. (alama 2)

17. iii) Huku ukitoa mifano mitatu onyesha tofauti iliyoko kati ya mazungumzo haya na mazungumzo yanayoweza kutokea mahakamani. (alama 3)

b) atatizo ya lugha katika matamshi yafuatayo yanasababishwa na nini? Andika lugha sanifu

(i) Nipeko jai nikunyenge wakati nikikungojeanga (alama 1)

(ii) Tsambi sangu sote simeoswa na tamu ya Yesu. (alama 1)

(iii) Alienda kukojoa baada yake kuhara. (alama 1)

iv) Mimi ninakuja kwa hapa. (alama 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA I

KISWAHILI 102/2

1. a) i) Haki za watoto

ii) Kutetea watoto

iii) Hatua za kulinda watoto n.k. 1x2

b) Dhiki za watoto zitaisha baada ya kutiwa saini kwa haki za watotot na umoja wa mataifa

1x2

c) Ni kuwapa watoto wachanga kazi zinazozidi nguvu na akili zao kinyume na sheria1x2

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

d) Kazi husumbua kukua kwa akili na mwili wa mtoto, na pia huvuruga maadili ya mtoto1x2

e) Uhuru ndio mwanzo wa maendeleo ya mtoto, hivyo bila uhuru mtoto hawezi kuendelea Al 2

f) Mtoto atasaidiwa na elimu, vyombo vya habari ili kuweza kupanua akili yake Al 2

g) Msingi mkubwa wa maendeleo ni elimu Al 1

h) i) Takribani- idadi inayokisiwa Al

ii) Tia saini- Weka idhini ya makubaliano Al 1

2. MUHTASARI/ UFUPISHO (Alama 15)

i) - Uhalifu ni wa mtu, mali au umma

ii) - Uhalifu wa mtu ni kama mauaji

iii) - Uhalifu wa mali ni kama wizi

iv) - Uhalifu wa kimaadili ni kama kamari

v) - Uhalifu unaohusisha usalama wa umma

vi) - Adhabu kwa uhalifu ni kifungo gerezani n.k. (7x2=14+1 ya mtiririko)=15

3. MATUMIZI YA LUGHA

Mwongozo wa kusahihisha

a) i) Hukuugua malaria

ii) Sijajenga kasri

b) i) Ugonjwa

ii) Ulezi n.k

c) i) Safari, msafara, msafiri, usafiri, usafirishaji

ii) Pendo, penzi, mapenzi, mpenzi

d) i) Chaka la waridi halizai ua jeusi

ii) Aliniandikia waraka mrefu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

e) - Ote: bila kubaki; ujumla wa kitu/ vitu; hakuna majalio; idadi kamili imetajwa

- O-ote: kila kitu; bila kuchagua au kubagua

f) i) Sawasawa

ii) Nabii Musa!

g) i) Mazrui alitaka kujua ni kwanini mabasi yalikuwa hayapiti hapo siku hizo

ii) Karen alimsihi Kadzo asiukanyage mguu wake, naye Kadzo alishangaa ikiwa angemkanyaga

h) Jinsi

i) Njia ya kutekeleza jambo

ii) Mwenendo

iii) Aina

Ikiwa

i) Kiunganishi

ii) Kama/ pengine

i) i) Mbao zetu zote zimeliwa na mchwa

ii) Sijali hata kama hunichukii

j)

Fa-	Fia	Fiana
Cha	Chea	Chana

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

k) Mtoto huyu alikunywa maziwa mengi

S

KN_1 KT

N V T KN_2

N_1 V_1

Mtoto huyu Alikunywa Maziwa mengi

(*Asipochora matawi apoteze alama 2)*

l) i) Sikununua gari kwa sababu sikupandishwa madaraka

ii) Nikipandishwa madaraka nitanunua gari

m) i) ni- ya kuonyesha wingi

ni- ya kuonyesha undani / mahali ndani

n) i) ndiye- kitenzi kishirikishi kipungufu

ii) amekuwa- kitenzi kisaidizi au kitenzi kishirikishi kikamilifu

o) i) Kata bei- amua bei ya mwisho ya kitu/ bidhaa / punguza bei

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ii) Tia ngoa- tia wivu

b) i) Mkungu- ndizi – Mkunga wa ndizi

ii) Thurea- nyota – Thurea ya nyota

c) i) Sarafu- shilingi/ peni

ii) Daktari- tabibu/ mganga

4. **ISIMU JAMII**

a) i) Muktadha

haya ni mazungumzo ya dini Al 1

ii) - Mada inayozungumziwa ni ya kidini

- Mambo yanayojadiliwa ni ya kimaadili

- Msamiati uliotumika ni wa kidini Al 2

iii) - Msamiati unaotumika hapa ni wa kidini kwa mfano; Amen, ibilisi na Bwana,

ilhali msamiati wa mahakamani ni wa kisheria kwa mfano; hakimu, hukumu na hatia

- Mazungumzo ya mahakamani huendelezwa kwa kufuata mandiki yaani mtiririko maalum. Mazungumzo ya kidini huendelezwa kwa mandiki inayoamuliwa papo hapo na wazungumzaji wenyewe

- Matumizi makubwa ya istilahi za urasmi kwa mfano; taarifa, daawa n.k. Katika mazungumzo ya kisheria hali ambayo haipatikani kwa mazungumzo ya kidini

Al 3

b) i) Tatizo la kupuuza mofu za Kiswahili na kuongeza zile za lugha ya mama Al ½

-Nipe chai ninywe huku nikikungoja Al ½

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ii) Tatizo la sauti aliyoizoea mtu katika lugha yake na haipatikana katika lugha ya Kiswahili

Al ½

- Dhambi zangu zote zimeoshwa na damu ya yesu Al ½

iii) Tatizo la adabu na kaida za lugha Al ½

- Alienda haja ndogo baada ya kuendesha Al ½

iv) Tatizo la muundo wa sentensi- Sintaksia Al ½

- Nitakuja hapa Al ½

KARATASI YA II

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

UFAHAMU (ALAMA 15)

1. **Soma tarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Jamii yoyote ile ulimwenguni haiwezi kukua, kuimarika na kuendelea bighairi ya kuwatunza na kuwaenzi watoto wake. Watoto ni mbegu ya jamii ya kesho na kama mbegu hiyo haikutunzwa ipaasavyo jamii ya kesho haitakua na endapo itakua itadumaa na kushindwa kuendelea. Ili kuhakikisha kuwa watoto wametunzwa ipasavyo, inaijuzu jamii nzima kufanya kulihali kuhakikisha kuwa watoto wake wamepata elimu ifaayo, afya inayowastahiki, ulinzi murua na usalama unaostahili. Jamii hiyo lazima ithamini haki za kibinadamu alizo nazo mtoto.

Serikali zote uilmwenguni zinapaswa kuthamini na kuenzi Muafaka kuhusu Haki za Mtoto. Nchi nyingi ulimwenguni zimekwisha kuafiki Muafaka kuhusu haki za mtoto. Muafaka huo unahakikisha kuwa zinaridhia kuhakikisha kuwa haki za mtoto hazitakiukwa na endapo zitakiukwa ziko tayari kukubali ukiukwaji huo mbele ya jumuiya ya ulimwengu mzima. Muafaka huo unashadidia haki za kimsingi za mtoto popote pale na bila ya ubaguzi. Haki hizi ni haki ya kuishi, haki ya kujiendeleza ipasavyo; haki ya kulindwa dhidi ya taathira mbaya, kudhalilishwa au unyanyasaji wa jinsi yoyote ile; kushiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa pamoja na dhidi ya kongwa la ajira.

Katika mataifa mengi, watoto wamesakamwa na wingi wa matatizo. Mathalan, kusokomezwa kwenye vita vya kikabila, ajira ya watoto, unyanyasaji wa kijinsia na maovu mengine ya ukiukwaji wa haki za kibinadamu. Zipo nchi ambapo watoto wanaoishi katika maeneo ya mashambani wana fursa chache za kupata elimu ifaayo na afya ya kimsingi wakilinganishwa na wenzao wanaosakini katika maeneo ya mijini. Muafaka huu unasisitiza kuwa kuwepo kwa tofauti za jinsi hii katika jamii ni ukiukaji wa haki za kibinadamu. Inahalisi serikali za nchi hizo kuhakikisha kuwa hali hizi zimefilia majinani.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

SEHEMU YA A: UFAHAMU ALAMA 15

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuatia

(a) Kwa nini jamii ya kesho inategemea hali nzuri ya watoto? (alama1)

(b) Ni hatua gani kuu ambazo zafaa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa watoto wanatunzwa ipasavyo? (alama4)

(c) Eleza haki zozote mbili za kimsingi walizo nazo watoto. (alama4)

(d) Taja dhiki wanazokumbana nazo watoto. (alama3)

(e) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika kifungu: (alama 3)

(i) bighairi ya

(ii) Kufanya kulihali

(iii) Kongwa la ajira

MUHTASARI

2. Soma taarifa hii kisha ujibu maswali:

Ukeketaji ni mfumo wa upasuaji unaofanyiwa wanawake na wasichana sehemu nyingi duniani. Istilahi hii ya ukeketaji ina maana pana kwani inaweza kutumiwa kuelezea upashaji tohara kwa wasichana na ukataji wa sehemu za siri kwa wanawake.

Ukeketaji haupatikani tu katika bara la Afrika bali katika sehemu nyingi ulimwenguni. Umri ambapo ukeketaji hufanyika hutegemea jamii inayohusika. Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza. Miongoni mwa jamii ambazo hupasha tohara wanawake, huthamini sana amali hii kwani kwao ni hatua muhimu ya mpito wa maisha

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

katika jamii za jadi mwanamke hupitishwa kutoka rika moja hadi lingine, yaani kutoka utotoni na kuingia kwenye utu uzima. Ukeketaji unafungamana na sherehe ya kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa. Dhima kuu ya sherehe hiyo ya kuwapasha wasichana tohara inadaiwa ya kwamba ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira. Jamii nyingine hutekeleza tohara kwa sababu za kidini zinazoshikilia kuwa mwanamke aliyetahiriwa huwa nadhifu. Wengine wanaamini kuwa tohara huwafanya watoto wanapozaliwa kuwa na nafasi nzuri ya kuishi, ilhali wengine hupashwa tohara ili wapate waume wa kuwaoa. Kwenye jamii ambazo wanaume wanasisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa ukeketaji umeshamiri. Katika jamii kama hizi wanaume huwa hawataki kuoa wanawake ambao hawajatahiriwa.

Wanawake wenyewe huhakikisha ya kwamba watoto au wajukuu wao wanapelekwa kupashwa tohara. Wakati mwingine mipango ya siri hupangwa na kina mama hao pamoja na mangariba, kuhakikisha kuwa jambo hili linatekelezwa. Kwa hivyo jambo hili la ukeketaji lina utata miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni.

Hata hivyo ukweli ni kwamba swala zima hili la ukeketaji lina madhara makubwa na linamdhalilisha mwanamke. Katika hali ya upashaji tohara wanawake huvuja damu nyingi na aghalabu huaga dunia. Wale wanaopona huwa kwenye hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa ambayo huharibu sehemu za uzazi. Kwani madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu.

Kwa sababu tohara hufanywa mara moja kwa mwaka, wasichana wote wa rika moja hukusanyika mahali maalum ili kufanyiwa tohara. Kifaa ambacho hutumiwa sana ni wembe. Wembe huo hutumiwa kuwakatia wasichana wote ambao wanapashwa tohara katika kipindi hicho. Wembe huo hauchemshwi anagalau kuua viini vinavyosababisha na kueneza magonjwa mbalimbali. Hali hii huwaweka wasichana

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

hao kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Licha ya hivyo wasichana waliotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua. Kwa hivyo wanaweza kupata magonjwa mengine ya kuambukiza kwa urahisi. Kwa hivyo ukeketaji ni tendo la hatari na la kumdhalilisha mwanadamu ambalo linastahili kulaaniwa.

(a) Ukizingatia mambo muhimu anayoeleza mwandishi, fupisha aya tatu za kwanza.
Maneno (60-70) (alama 9)

Nakala chafu.

Nakala safi.

(b) Eleza mambo anayoeleza mwandishi katika aya mbili za mwisho. Maneno 40-50 (alama 6)

Nakala chafu.

Nakala safi.

MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

3. a) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi**.** (alama 2

(i) Sujudu

(ii) Haribu

(iii) Hiliki

(iv) Abiri

b) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye maneno haya. (alama 4)

(i) Karatasi

ii)Samahani

c) **Akifisha kifungu kifuatacho** (alama 3)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Karibu mgeni akaitikia mwenyeji mbona huingii na mlango u wazi naam stareheni kwenye kiti ahsante wakajibu.

d) **Andika sentensi hizi kwa udogo.** (alama 2)

(i) Mlete huyo mwizi afunguliwe mashtaka.

(ii) Sijui kwa nini hindi lake ni bichi

(e) **Andika sentensi hii kulingana na maagizo.** (alama 2)

Chombo kilichozama kiliandikishwa uingereza.

(Maliza kwa kiliandikishwa)

(f) **Onyesha kinyume cha vitenzi vifuatavyo.** (alama 2)

(i) Epua

(ii) Tapanya

(iii) Nena

(iv) Unga

(g) **Kanusha** (alama 3)

(i) Chovi angekuwa na bidii angependwa na wengi.

(ii) Kilima kwake kulisifiwa sana.

(iii) Ukicheza na moto utachomeka.

h) **Geuza kwa wingi.** (alama 2)

(i) Njia hii huenda Kisumu

(ii) Wembe huu utafaa.

i) **Tumia kauli ya kutendesha katika sentensi zifuatazo:**. (alama 2)

(i) Mukhwana alikunywa pombe mpaka akalewa sana

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(ii) Tafadhali hakikisha Omari ameelimika vizuri

j) **Changanua sentensi hii.** (alama 4)

Watoto wanafanya kazi zao lakini wazazi wanazungumza sana.

k) **Geuza katika msemo wa taarifa.** (alama2)

"Lo! Siamini kuwa yule mtoto aliyetaabika vile ameishia kupata udhamini" Alisema Mariamu

l) Sahihisha sentensi zifuatazo. (alama2)

i)Hao mandugu wamekosana juu ya pesa.

ii) Mtu mwenye anakula mkate ametumana aletewe chai.

m) **Eleza matumizi ya KWA katika sentensi zifuatayo:** (alama 2)

(i) Wanawake kwa wanaume walifika mkutanoni.

(ii) Yule mtaalam alielezea maana ya utandawazi kwa ufasaha.

n) **Fafanua maana mbili zinazojitokeza katika sentnsi hii.** (alama 2)

Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.

o) **Tunga sentensi kubainisha maana tofauti ya maneno haya;** (alama 2)

i) Dalili

ii) Dhalili

p) **Toa neno jingine lenye maana sawa na;** (alama3)

i) Karadha

ii) Mtaji

iii) Mshitiri

q) **Eleza maana ya misemo hii.** (alama2)

i) Umbo la mkonge

ii) Kupata hiji wa hoja

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

r) **Eleza maana ya methali ifuatayo:** (alama2)

Akikalia kigoda mtii.

SEHEMU YA D. ISIMU JAMII (alama10)

4. Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

"Karibu wageni karibuni

Come and learn with us lugha ya kiswahili.

Nyote mtabenefit sana"

"Kwa nini?"

"Kwa sababu its a national language"

a) Lugha ngapi zimetumika katika muktadha huu?

b) Mtindo wa kutumia lugha zaidi ya moja katikia mazungumuzo huitwaje?(alama2)

c) Eleza sababu za wazungumzaji kutumia lugha zaidi ya moja. (alama5)

d) Mzungumzaji mwenye uwezo wa kutumia lugha zaidi ya mbili anaitwaje?(alama2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA II

KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

1. 1 a) Watoto ni mbegu ya kesho/ watoto huendeleza kizazi

b) Kuthamini na kuenzi muafaka kuhusu haki za watoto. Apate

Elimu ifaayo

Afya inayowastahiki

Ulinzi na usalama unaostahiki

c) -Haki ya kuishi

-Kujiendeleza ipasavyo

-Kulindwa dhidi ya taathira mbaya

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

-Kushiriki katika maisha ya kijamii, kiuchumi, kisiasa

-Elimu

d) Dhiki

-Vita vya kikabila

-Ajira ya watoto

-Unyanyasaji wa kijinsia

e) i) Bila ya kujali;

mbali na

ii) Kwa vyovyote vile

kwa kila namna

iii) Utumwa wa ajira ya watoto

MUHTASARI

2. a) - Ukeketaji ni upasuaji unaofanyiwa wasichana na wanawake.
- Hupatikana barani Afrika na sehemu nyingi ulimwenguni.
- Umri ambapo ukeketaji hufanyika hutegemea jamii
- mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza
- Jamii huthamini amali hii kwani ni hatua ya mpito wa maisha
- Hufungama na kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa
- Dhima kuu ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira
- Wanaume husisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa
- Wanawake wenyewe huhakikisha watoto au wajukuu wanapashwa tohara

b) - Ukeketaji una madhara na unadhalilisha wanawake

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Wanawake huvuja damu na aghalabu huaga dunia
- Wale wanaopona huwa na hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa
- Madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu
- Wembe utumiwao hauchemshwi kuua viini
- Wasichana wanaotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua
- Ukejetaji humdhalilisha mwanamke na linastahili kulaaniwa

SEHEMU YA C: MATUMIZU YA LUGHA (ALAMA 40)

3. a) i) -Sijida

ii) -Harabu, Uharibifu, Uharibikaji, Mharibifu

iii) -Hidaki

–Abiria Alama 2

b) i) Karatasi/ Kara'tasi

ii) Samahani/ Sama'hani alama 1

c) " Karibu mgeni ". Akaitikia mwenyeji. " Mbona hauingii na mlango u wazi? " "Naam stareheni kwenye viti . " "Asante . " Wakajibu.

d) i) Kilete hicho kijizi kifunguliwe mashtaka

ii) Sijui kwanini kihindi chake ni kibichi alama 2

e) Uingerza ndiko/ ndipo chombo kilichozama kiliandikikishwa Alama 2

f) i) Epua-Teleka

ii) Tapanya-Kusanya

iii) Nena- Nyamaza

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

		Unga-Kata/ tenga/ pinga	Alama ½ x4=2
g)	i)	Chovi asingekuwa na bidii asingependwa na wengi	
	ii)	Kutolima kwake hakukusifiwa sana	
	iii)	Usipocheza na moto hutachomeka	Al. 1 x 3 = 3
h)	i)	Njia hizi zaenda/ zinaenda Kisumu	
	ii)	Nyembe hizi zitafaa	Al. 1 x2 =2
	i)	Pombe nyingi aliyoinywa Mukhwana ilimlevya sana	Alama 1
	ii)	Tafadhali mwelimishe Omari vizuri	Alama 1
j)	-	Watoto-nomino (N_1)	
	-	Wanafanya kitenzi (T_1)	
	-	Kazi nomino (N_2)/ shamirisho kipozi	
	-	Zao-Kivumishi kimikilishi (V)	
	-	Lakini Kiungamishi (U)	
	-	Wazazi-nomino (N_3)	
	-	Wanazungumza-kitenzi (T_2)	
	-	Sana-kielezi/ kiarifa/ chagizo	Alama ¼ x 8=2
k)	Mariamu alishangaa na kutoamini kuwa yule mtoto aliyetaabika vile alikwisha kupata udhamini		Alama 2
l)	i)	Hao ndugu wamekosana kuhusu pesa	
	ii)	Mtu anayekula/ ambaye anakula mkate ametuma aletewe chai	Al. 1 x2 =2
m)	i)	Pamoja na	
	ii)	Namna/ jinsi	Al. 1 x2 =2

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

n) - Jambazi aliiba gari jipya la Okoth

- Jambazi aliiba gari jipya na kumpa Okoth Alama 2

o) i) Dalili-ishara/ alama

ii) Dhalili-Dunisha/ shusha hadhi/ shusha thamani Alama2

p) i) karadha-Hasara

ii) Mtaji-Raslimali

iii) Mshitiri – mteja / mnunuzi Al. 1 x3 = 3

q) i) Umbo la mkonge- Urafiki wa kujifanya mwema kumbe anaweza kukuangamiza

ii) Kupata hiji wa hoja-Kupata bahati/ kunusurika Alama2

r) Mtu yeyote mwenye uwezo au mamlaka ya namna Fulani anapaswa kuheshimiwa Alama 2

. a) Lugha mbili/ Kiswahili na Kiingereza Alama1

b) Kuchanganya na kubadili msimbo/ ndimi mseto/ kuchanganya ndimi - Alama 2

c) -Umahiri wa lugha zote mbili Alama 5

-Kujinasibisha na tabaka fulani aghalabu la juu

-Msemaji kukosa msamiati au lugha anayotumia kukosa msamiati

-Ari ya kutaka kueleweka zaidi

-Kutenga au kushirikisha watu

d) Bilinguo/ bilingua Alama 2

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA III

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

UFAHAMU

1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia: (JUMLA ALAMA 15)

Nchi yetu imeraukia mawio ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya Uchaguzi kukosa kuendeleza uchaguzi kwa njia iliyostahiki. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Hivi sasa Wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya zaidi ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya Wakenya vimeshamiri na kupaaza sauti vikilalamikia kukosa makazi, lishe na hata ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya 'wenyeji' kuwatimua 'wageni' na damu kumwagika.

Misukosuko ya kisiasa kama hii imekumba mataifa mengi ya Afrika miaka nenda rudi na kuchangia bara kudumaa na kuvia kiuchumi.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbizi kutoka nchi jirani zinazokumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, zikiwemo Somalia na Sudan. Kinaya ni kwamba Wakenya wamekuwa wakimbizi katika nchi yao wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu.

Ukabila na tamaa ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyama vikuu vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila kila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine, viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wameamua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya Wakenya ni wakimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na Shirika la Msalaba Mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa Lakini, kuna tetesi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni Wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao.

Matukio kama haya hayastahili kutukia asilani katika taifa hili.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Twahitaji zao aali la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi. Wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikizia mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu udugu na utaifa. Fauka ya haya, masuala yanayohusiana na umiliki wa ardhi yanafaa kutadarukiwa kwa dhati.

Maswali ya Ufahamu

a. Toa anwani mwafaka kwa makala haya. (alama 1)

b) Taja madhara manne ya ukabila. (alama 2)

c) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekumbwa na changamoto gani? (alama 1)

d) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. (alama 2)

e) Mwandishi anatoa mapendekezo yepi kwa kutatua tatizo hili la ukabila. (alama 4)

f) Eleza kinaya cha maisha ya wanakenya kwa sasa. (alama 1)

g) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu.

a) Mawio
b) Kuvia
c) Aali
d) Tadarukiwa.

(Alama 4)

UFUPISHO

Soma makala haya kisha ujibu maswali yafuatayo.

HAKI ZA BINADAMU

Binadamu wana mazoea ya kufikiria kuwa jinsi wafanyavyo, waongeavyo na wafikiriavyo kuhusu vitu ndivyo inavyopasa kuwa. Kama binadamu tunaamini njia yetu ndiyo sahihi, yenye mantiki na inayopasa kufuatwa na kila mtu. Msingi huu huu unakwenda kinyume na kutambua kila binadamu ana haki ya kufikiri, kusema au kuongea na kutenda mradi asikiuke haki ya mwenzake iliyo sawa na yake. Nguzo mojawapo *inayogongomelea hoja* hii ni Haki za Binadamu.

Azimio la kutangaza Haki Bia za Binadamu liliafikiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10 Desemba, 1948. Baraza kuu hilo liliyasisitizia mataifa wanachama umuhimu wa kuyasambaza, kuenezea, na kusisitiza kusambazwa kwa azimio hilo katika shule na taasisi za kielimu. Msingi wa uhuru, haki na amani ulimwenguni ni kutambua binadamu wote wana haki sawa. Ingawa kimsingi jamii na mataifa yote ya ulimwengu yanapaswa kuthamini, kusambaza na kuhimiza umuhimu wa Haki za

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Binadamu zipo jamii ambazo hukiuka haki hizo. Matokeo ya ukiukaji huu yana athari hasi sana kama ilivyotokea nchini Rwanda na Bosnia. Herzegovina kulikotokea mauaji ya halaiki.

Azimio la Haki za Binadamu linajumuisha vipengele kadha ambavyo ni mihimili mikuu ya Azimio lenyewe. Kipengele msingi kabisa kinasisitiza kuwa kila kiumbe anazaliwa huru na ana haki na hadhi sawa na kiumbe mwingine. Ukweli wa kauli hii ulikokotezwa na kauli ya mwanafalsafa maarufu Jean Jacques Rosseau aliyesema kuwa kila kiumbe huzaliwa huru lakini huwa katika pingu ulimwengu mzima. Kauli hii ilitambua ukiukaji huu wa kipengele hiki. Kipengele cha pili kinasisitiza kuwa binadamu wote wana haki za kufurahia uhuru wao pasi na kutengwa au kubeuzwa kwa misingi yoyote ile si rangi, kabila, jinsia, lugha, dini, asilia, utajiri au chochote kile.

Vipengele vingine vinatukumbusha kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na kupata ulinzi. Hamna mtu anayepaswa kuishi maisha ya utumwa au unyonge wa kutumikishwa kwa namna yoyote ile. Suala hili linasisitizwa na kipengele cha sita kinachokataza kudhalilishwa kwa watu au kutunzwa kwa namna yoyote ambayo inamfedhehesha kama kiumbe. Azimio la Haki za Binadamu linasisitiza kuwa binadamu yoyote yule ana haki ya kupata ulinzi wa kisheria. Binadamu huyo hapasi kubaguliwa na ana haki ya kupata fidia ya kisheria taraa haki zake za kimsingi zikikiukwa.

Hata hivyo sio watu wote ulimwenguni ambao wanazifurahia haki hizi za kimsingi. Zipo *lukuki za jamii* ulimwenguni ambako haki za kimsingi zinakiukwa. Katika nchi ambazo zinaongozwa na watawala wa kiimla, si ajabu kuona haki za binadamu zikikiukwa. Viongozi wa aina hiyo huwa wamegeuzwa ng'ombe wa shemere na tamaa, ubinafsi na ukatili usiojua thamani ya utu. Viongozi wa aina hii wanasahau kuwa kila binadamu ana haki ya kuishi maisha huru, asipotumikishwa wala kulanguliwa kama bidhaa.

Nchi za kiimla aghalabu huongozwa na itikadi kuwa kiongozi ndiye pekee ambaye ana uwezo wa kufikiri, kuamua na kutenda. Watu wengine wanapaswa kumfuata kisilka kama yule mbwa wa Pavlov ambaye alitokwa na mate kila kengele ilipopigwa. Viongozi wa aina hii hawachelei *kuwatenza nguvu* raia zao; kuwadhalilisha kwa namna nyingi. Viongozi wa aina hiyo huiona sheria ya nchi kama iliyowekwa kwa watu wengine bali sio wao.Msimamo huu unakwenda kinyume na kipengele cha saba cha Haki Bia za Binadamu kisemacho kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

Baadhi ya haki zinazokiukwa katika jamii za kimabavu ni haki ya watu kuungana, kuwaza, kushiriki katika maamuzi ya serikali, kuwa mwanachama wa jumuia waitakayo, kumiliki mali, kutembea, kuishi anakotaka, kutohukumiwa bila ya kuwako na utaratibu wa kisheria. Ni muhimu hata hivyo kujua ni muhimu kwa raia wenyewe kujielimisha na kuzijua haki zao. Serikali inapaswa kuwa mlinzi wa sheria zenyewe. Lakini muhimu kujua pia kuwa mlinzi naye hulindwa pia.

a) Kwa maneno kati ya 90 – 100 fafanua Haki Bia za Binadamu zilizoafikiwa na Baraza kuu la umoja wa Mataifa. (Alama 10)

Nakala Chafu

Nakala Safi

b) Kwa nini viongozi wa kiimla hukiuka haki za binadmu. (Maneno 50 -60).

Nakala Chafu **(Alama 5)**

Nakala Safi

III SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

1. **Andika methali inayoafikiana na maelezo haya**

   Kwa kawaida, mtu hupendelea nafsi yake (alama 2)

2. **Andika katika udogo**

   Mwanamke alimuua mbuzi kwa shoka. (alama 2)

3. **Weka shadda katika neno 'barabara' ili kuibua maana tofauti ya neno hilo**

   i) Barabara (maana)

   ii) Barabara (maana)

4. **Tunga nomino mbili kutokana na vitenzi hivi. Hakikisha viko katika umoja. (Alama 2)**

Kitenzi	**Nomino**	**Nomino**
Elewa		
Suka		

5. **Onyesha mofimu katika neno lifwatalo na utaje ni za aina gani**

   Kilichowaumiza. (alama 3 ½)

6. Tunga sentensi yenye mpangilio huu wa kisarufi. (alama 2 ½)

   I + W + T + N + V.

7. **Tunga sentensi kudhihirisha maana tofauti kati ya**

   (a) Jozi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(b) Njozi (alama 2)

8. **Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa.**

"Ninataka kumwona askari aliyemletea mfungwa tupa sasa hivi," alisema Batu. (alama 2)

9. **Eleza na uonyeshe matumizi manne tofauti ya kiambishi 'ku'** (alama 4)

(i) ……

(ii) ……..

(iii) …….

(iv) …….

10. **Kanusha sentensi hii katika wingi**

Mgonjwa mwenye kichomi aliyelazwa hospitalini ameaga dunia. (alama 2)

11. Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi na useme ni sentensi ya aina gani

Wale wanafunzi stadi walioibuka na alama bora zaidi, wameajiriwa kazi.

a) Aina …….. (alama ½)

b) Mchoro (alama 7 ½)

12. Onyesha virai vitatu katika sentensi hii na utaje ni vya aina gani.

Mtoto yule mdogo amekunywa maziwa kwa kikombe. (alama 3)

(i)……

(ii)……

(iii)……

13. Tunga sentensi tatu ukitumia neno papara liwe na sifa hizi. (alama 3)

a) Kielezi

b) Nomino

c) kivumishi

14. Sauti hii hutamkiwa wapi na huitwaje?

|Ch| (alama 1)

IV ISIMU JAMII. (alama 10)

(a) Jadili sifa tatu kuu za lugha ya taifa. (alama 3)

b) Eleza majukumu saba ya lugha za taifa. (alama 7)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA III

KISWAHILI 102/2

1. Ufahamu

a) Machafuzi ya uchagusi
misukosuko ya kisiasa
au jibu lolote mwafaka – **alama 1**

b)

- Wakenya kukosa makazi
- Kukosa lishe
- Ndoa kusambaratika
- Kumwagika kwa damu
- Uchumi kuzorota **½ x 4 = 2**

c)

- Ubaguzi kwa misingi ya kikabila katika ugawaji wa misaada **alama 1**

d) Vita katika Somalia vinasababishwa na koo zinazopigania uongozi ilihali Kenya vinasababishwa na ukabila na tama ya uongozi alama2

e) Viongozi wawe watumishi wa wananchi bali wasijilimbikizie mali na kungangania uongozi

- Katiba irekebishwe
- Wakenya waelimishwe kuhusu udugu na utaifa
- Masuala ya umiliki wa mashamba yashughuilikiwe **1 x 4= 4**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

f) Wakenya kuwa wakimbizi katika nchi yao ilihali awali waliwahifadhi wakimbizi kutoka nchi jirani

alama 1

g) i) Mawio- mwanzo wa machafuzi

ii) Kuvia- Kuzorota / kukosa kuendelea / kudumaa/ Kosa kuendelea

iii) Aali- bora / tukufu / wanaofaa

iv) Tandarukiwa- shughulikiwa

11 SWALI LA PILI (UFUPISHO)

1. Kwa maneno kati ya 90- 100 fafanua Haki Bia za Binadamu Zilizoafikiwa na Baraza kuu la Umoja wa mataifa

- Kila kiumbe anazaliwa humu na ana haki na hadhi sawa na kiumbe mwingine'
- binadamu wote wana haki za kufurahia uhuru wao pasi na kutengwa au kubeuzwa kwa misingi yoyote ile si rangi, kabila jinsia, lugha , dini, asilia au chochote kile
- Kila mtu ana haki ya kuishi na kupata ulinzi
- Hamna mtu anayepaswa kuishi maisha ya utumwa , kutumikishwa , kudhalilishwa au kutunzwa kwa namna inayomfedhehesha kama kiumbe
- Haki ya kupata ulinzi wa kisheria
- Kutobaguliwa an ana haki ya kupata fidia ya kisheria taraa haki zake za kimsingi zilikiukwa

Alama 8 utiririko alama 2)

11. Kwa nini viongozi wa kiimla hukiuka haki za binadamu

- Tama ya uongozi
- Ubinafsi
- Ukatili, hawajui thamani ya utu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Kiburi cha kujiona kuwa wao ndio wanaofahamu mambo zaidi
- Husahau kuwa binadamu ana haki ya kuishi maisha huru bila kutumikishwa au kutanguliwa kama bidhaa
- Hudhani wao tu ndio wana uwezo wa kufikiri, kuamua na kutenda na wananchi wanapaswa kufuata tu
- Huona kuwa sheria ya nchi imewekewa wengine na wala sio wao hivyo huwatenza uguvuraia zao

Alama 4, utiririko alama 1)

III SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Mwongozo wa kusahihishia

1. Kila mwamba chumvi huombeya chunguche
   Kila mwamba ngoma huvutia kwake
2. . Kijanajike kilikiua kibuzi kwa kishoka **½ x 4 = 2**
   ½
3. Barabara _____Njia (Nomino) ✓ alama 1
   ½
   Barabara _____Kama inavyotakiwa ✓alama 1
   (Kielezi) **alama 3**
4. Kitenzi Nomino Nomino✓
   Elewa Mwerevu✓ Uerevu✓
   Suka Msusi ✓ Ususi
   ½ x 4 = 2
5. Mofimu kilichowaumiza
   ✓Ki_____ kiambishi cha ngeli ✓ ½

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Li_____	wakati uliopita ✓	½ **x 7 = 3** ½
Cho____	Kirejeshi ---O—	
Wa_____	kitendwa / mtendwa	
Um_____	mzizi wa kitenzi / shima	
IZ_____	kauli ya mnyambuliko ya kitendeshwa	
A_____	kilishio	
		½ x 7= 31/2

6. Ala! ✓ Wewe ✓ umemla ✓ mbuzi✓ mzima✓ **½ x 5= 21/2**

7. Jozi---------- maana , vitu viwili vilivyo pamoja na vinavyofanana

   Njozi – Ruya, ndoto

_ _Mwanafunzi atunge sentensi asitolee maana tu!

8. Usemi wa taarifa

   Batu alisema kuwa ½ alitaka kumwona askari aliyempelekea ½ mfungwa tupa wakati , ½ ule, ½ ule.

9. _____Matumizi manne ya kiambishi ku

a) Vitenzi jina ------- Kuimba kwaka ni kuzuri ✓

b) Kiwakilishi cha nafsi ya pili umoja (wewe) ✓

   Amekulalamikia kwa nini?

   Ninakutaka ufike hapa

c) Kiwakilishi cha mahali✓

   Kuliko na misitu kuna wanyama wengi sana ✓

d) Katika kukanusha wakati uliopita

   Omolo alioa jana-Omari hakuoa jana **1x 4= 4 alam 4)**

10 Mgonjwa asiye ✓ ½ na kichomi hakulazwa ✓ ½ hospitalini

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

na✓ ½ hajaaga dunia ½ x 4 = 2 alama

11 a) Sentensi changamano (Al ½) Aina ya sentensi

b) Mchoro

S✓

KN KT✓

W✓	N✓	V✓	S✓	T✓	N✓
Wale ✓	wanafunzi✓	stadi✓	walioibuka Na Alama bora Zaidi ✓	wameajiriwa✓	kazi ✓

15✓

½ x 15 = 7 ½ + ½ (Aina) = alama 8

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

12 Kirai Nomino — Mtoto yule

Kiria kivumishi — Yule mdogo

Kirai Kihusishi — Kwa kikombe

13 a) Kielezi

Alifanya kazi ile Papara akamwudhi Mwalimu wake

b) Nomino

Papara zako zitakutia mashakani siku moja

c) Kusoma papara huchukiza wengi

Nomino

Ya

kitenzi jina

14. CH

Wapi? Kwenye kaakaa gumu ½

Jina? Kipasuo kwamizo ½

ISIMU JAMII

a) Sifa za lugha ya taifa

i) Ina wazungumzaji wengi

ii) Ni lugha ya mama/ kwanza ya kikundi cha watu katika taifa husika

- Ili wapokezane utamaduni
- Ili wafunze wengine

iii) Iwe na muundo wa kiisimu unaofanana na ule wa baadhi ya lugha za watu katika lugha husika hivyo kujifunza ni rahisi K.M Kiswahili na lugha zingine za kibantu K.v kiluhya , Kikuyu n.k

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ii) iv) Iwe lugha mojawapo asilia, isiwe ya kigeni bali ya kienyeji; isilete chuku bali ieleze hisia za uzalendo na utaifa **yoyote 3 x1 = 3**

b) Majukumu ya lugha za taifa

i) Huleta umoja wa taifa lote/ huunganisha watu

ii) Huwawezesha kufanya kazi kwa pamoja kwa manufaa ya taifa

iii) Ni kifaa cha kuziba mipaka ya kikabila

iv) Hukuza utamaduni wa kiafrika kwa sababu hutumika na watu wa makabila tofauti lugha hubeba utamaduni wa watu k.m utamaduni wa ujamaa Tanzania

v) Hukuza uzalendo wa watu wa taifa kwa kutumia lugha kama kifaa cha kuonyesha hisia za kizalendo

vi) Hutambulisha watu wa taifa Fulani kwa mfano; wimbo wa taifa n.k

vii) Huleta maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kisayansi kutokana na umoja wa taifa lugha

viii) Husawazisha watu kilugha kwani hisia zitakuwa sawa

ix) Husaidia kufananishaharakati za uongozi kutokana na kuhimiza matumizi ya lugha moja ambayo inarahisisha jukumu la serikali katika uongozi yoyote 7 x 1= 7

Hoja saba x 1= 7

7 x 1= 7

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA IV

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

1. **UFAHAMU**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Siku moja , mtu ambaye alijulikana kwa jina la Moto , alikuwa Ameketi chini ya kivuli cha mbuyu. Alikuwa akifanya hivyo kwa kungojea kulungu kunaswa na mtego wake. Hapo mbuyuni, ndipo palikuwa na njia ya kulungu ya kwenda mtoni kunywa maji. Kupitia mbuyuni, iliwabidi kwanza wapitie pale mtegoni. Lakini kwa kuwa kwa siku hii ya leo wakati wao wa kunywa maji ulikuwa bado kuwadia, naye Moto, badala ya kurudi ili aje baadaye, akaonelea heri angojee hapo.

Haikuwa mara yake ya kwanza kutega kulungu. Alikuwa amewanasa wengi na kwa muda mrefu sana. Na ingawaje alifurahia nyama yao laini, ni kuwachuna ndiko alikokuzira. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya vifaa butu vya mawe ya kuchonga alivyokuwa akitumia. Kwa sababu hii basi, haikuwa rahisi kuwachuna. Pia, alikuwa akiwala wabichi. Ili kujipa kazi akisubiri, akaonelea amtengenezee utunda mpenzi mkewe. Hakuwa na shida kuamua utunda huo ungekuwa wa namna gani. Nyakati hizo, shanga zilikuwa bado hazijavumbuliwa. Ni jiwe na mti tu ndivyo vilivyokuwapo, navyo ndivyo vilivyokuwa mali ghafi.

Kwa ala yake, jiwe la kuchonga, Moto akakata vijiti viwili. Kikubwa akakiita 'mama' na kidogo, 'baba'. Dhamira yake ilikuwa kumtengenezea mkewe ushanga na tembe zikiwa za mti. Akiweka kijiti mama chini, alitumia kijiti baba kupekejea tundu. Alifanya hivi kwa nguvu zake zote, Haja ilikuwa ni atoboe matundu mengi, halafu ayakate na kuyaviringisha na baadaye ayaunge na uzi wa muaa ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha, na jasho kumtoka, na huku mawazo yake yote yakiwa juu ya uso wa mkewe, hakuwa ameona cheche zikianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake. Alichokisikia kwa ghafla, kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika. Alishtuka na akaruka kwa woga. Hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani!

Huku akitetemeka kwa hofu, cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Sasa ikawa imepata nguvu na kuwa tsanzala ambayo ilienea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kuangalia hivi, akajiona amesimama peupe! Kutoka kwa

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

upande wa mtegoni, kukaja harufu nzuri ya kunukia. Alifuata na alipofika, akaona kulungu ambaye alikuwa ameshikwa na mtego, ameokwa vizuri sana na nguvu hizo ngeni. Hakujua zinaitwaje wala hakujua aziiteje. Kwa hivyo, hakuwa ameshawahi kuona ama kuonja kitu cha kuchoma sembuse cha kupikwa!

Ni harufu ya kuiva ya kulungu na kudondoka kwa mafuta ya kunona ndivyo vilimtia ujasiri. Naye kwa hatua za woga, akanyatanyata akanyakua kinofu na kukionja. Si utamu huo aliousikia! Sasa akanyafua jinofu. Halafu akaingilia maini, moyo na mafigo. Kulungu akamshinda ingawaje alimla maradufu ya kawaida yake. Aliyebaki, akamfunga ndani ya majani ya mgomba na kuwapelekea watu wake. Pamoja na kulungu, akawa amechukua pia kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili ambavyo baadaye kijiti mama alikuja kukiita "wimbombo" na kijiti baba, " ulindi"...

Ilikuwa alfajiri asubuhi watu waliposhitukia "tatata" za kualika kwa kuni na kulipuka kwa moshi kutoka nyumbani kwa Moto. Nyumba yenyewe ilionekana ikiwa na nuru nyekundu ya ajabu na ya kutisha. Walinyatanyata kuelekea kwenye kioja hicho. Kiliwavutia zaidi kwani walivyozidi kulisongelea, ndivyo ile baridi ya asubuhi ilivyozidi kuwatoka. Mvuto huo ukawapumbaza. Lakini walipumbazika zaidi walipoona - nyuma ya kioja hicho na kupita pazia la moshi, Moto ameketi.

Macho yake yalionekana mekundu mno. Hii ilikuwa sababu ya moshi; lakini hawakuwa wakijua hivyo. Kiwiliwili chake kilionekana kikiyumbayumba nyuma ya miale. Haya yote yakamfanya kutisha. Wenzake wasijue la kufanya kwa sababu ya bambuazi, wakawa wamesimama tuli wameduwaa. Hapo ndipo waliposikia sauti ikinena: "Mimi ndimo Moootoo...; naivisha na kuunguza, natokeza na naoteka. Anitakaye nitakuja kwake nimpe huu uwezo wangu..."

Ili kuwaogofya zaidi, akaupulizia nao ukaalika kwa moshi na cheche nyingi zilizowafanya wenzake kurudi nyuma kwa hofu. Kuona hivi, akaendelea kuwatia woga kwa kusema, "Hizi ndizo nguvu za Moootoo... mimi ndimi Moootoo...nijieni niwageuzie maisha yenu..."

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Akiwa bado ana sehemu ya nyama ya kulungu, akawagawia na kuwaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo aliwaambia siri ya kioja. Hakuwaambia ule ukweli wa mambo, badala yake, aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao, kwa kukosa jina la kufaa, wakaliita "Moto".

Punde si punde, watu wakawa wamezoea moto na wengi wakawa wanakuja kwake tu. Hakutaka uenee vivi hivi tu. Kwa hivyo, akaweka masharti: moto ulipatikana kwake tu kila jioni, na uzimwe mara moja baada ya matumizi. Ni hapo kwake tu ambapo "moto mpya" ungeweza kupatikana. Moto hauibiki wala haufichiki, akawakanya. Na ambaye angefanya ujasiri wa kuuiba ama kuuficha, basi asije kulia kwake baadaye, akawaeleza.

Masharti haya yalifuatwa, naye akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa - na punde si punde, za utukufu pia! Sasa watu wakawa, bila moto, hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi. Hapa ndipo aliwageukia na kuwaambia:

“Ili kuulinda huu Moto Mtakatifu usife, imenibidi kuacha kazi zangu. Lakini siko radhi kuendelea kufa njaa na familia yangu."

" Tutakugawia chakula chetu ili uzidi kuuchunga huo Moto Mtakatifu ili usife," wakamkatiza.

Basi, kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Siku si nyingi, mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto", ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha na kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "Utukufu wa Moto".

Maswali

a) Ipe makala uliyoisoma anwani mwafaka (alama 1)

b) Moto alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu kwa sababu gani? (alama 2)

c) Ala za pekee za wakati huo zilikuwa zipi**?** (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

d) Uvumbuzi wa Moto ulikuwa na athari zipi katika maisha ya jamii? (alama 2)

e) Kwa kutotaka Moto uenee hivi hivi tu, Bwana Moto aliuwekea masharti. Taja mawili (alama 2)

f) Moto na Aila yake walifaidikaje baada ya ufumbuzi huu? (alama 2)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 4)

(i) Kioja

(ii) Alikokuzira

(iii) meza kichaka

(iv) wimbombo

UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha uiibu maswali yanavofuata.

UGONJWA wa utando wa ubongo ambao kwa kiingereza unafahamika kama *meningitis* huzua hofu miongoni mwa watu wengi. Ugonjwa huo pia hujulikana kama homa ya uti wa mgongo.

Hofu kama hizo zinaeleweka kwa sababu utando wa ubongo ni ugonjwa unaoathiri ngozi inayofunika ubongo na uti wa mgongo na kwa hivyo ni rahisi mno kusababisha kifo ikiwa mgonjwa hatahudumiwa haraka iwezekanavyo.

Utando wa ubongo ni ugonjwa unaosababishwa na virusi na bakteria, Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, utando wa ubongo unaosababishwa na virusi sio hatari sana kwa uhai wa mtu ikilinganishwa na bakteria. Japo watu wengi wanaougua utando wa ubongo hutibiwa na kupona, baadhi yao huachwa wakiwa bubu au vipofu na wengine kufariki.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Shida kubwa ya ugonjwa huu ni kwamba unatokea bila kutarajiwa. Kwa mfano mtoto au mtu wa umri mkubwa anaweza kuwa mzima kwa muda wa dakika kadha ila baadaye kuwa mgonjwa mahututi baada ya kukumbwa na ugonjwa huo. Shida nyingine ya ugonjwa huu ni kwamba huwa vigumu kutenganisha dalili za ugonjwa huu na dalili za magonjwa mengine ya kawaida kama vile maumivu ya kichwa. Kwa hivyo kuna baadhi ya watu wanaomeza dawa za kupunguza maumivu ya kichwa bila kujua wanaugua utando wa ubongo.

Dalili za watoto wanaougua utando wa ubongo ni homa, kutapika, mtoto kukataa kula na kulia kwa uchungu. Mtoto anayeugua ugonjwa huu kadhalika huwa anaonyesha dalili za kufura kichwa, kupumua kwa haraka na kutupatupa miguu huku mwili wake ukiwa umejikunyata. Watu walio na umri mkubwa nao huonyesha dalili za maumivu makali ya kichwa, kuwa na shingo nzito (stiff neck) na mgonjwa kuepukana na mwangaza. Kadhalika mgonjwa hushikwa na homa na pia kutapika kando na kukosa ufahamu.

Utafiti umeonyesha kwamba watu walio na umri mkubwa kadhalika huonyesha dalili za kuwa na mikono au miguu baridi, maumivu ya misuli na tumbo hasa kutokana na damu kuwa na sumu. Ni muhimu kufahamu kwamba sio kila mtu anahisi dalili hizi, ikiwa yeyote atashuhudia baadhi ya dalili hizi itakuwa bora kufika hospitalini haraka kupata usaidizi wa daktari kabla ya ugonjwa huo kuzidi sana.

Yeyote anayeshuku kwamba anaugua utando wa ubongo anapaswa kupelekwa hospitalini mara moja. Hii ni kwa sababu ni rahisi mno kwa madaktari kutibu mgonjwa anayepelekwa hospitalini punde tu anapoonyesha dalili ikilinganishwa na yule anayepelekwa huko kama amechelewa.

Maswali

a) Bila kubadilisha maana fupisha aya nne za mwanzo (Maneno 70-80)

(alama 7, 1 ya utiririko)

Matayarisho

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Nakala safi

b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, eleza dalili za ugonjwa wa utando wa ubongo na huduma kwa mhasiriwa (Maneno 55-65) (alama 6, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

2. .MATUMIZI YA LUGHA

(a) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli zipi**?**

i) neno ……

ii) mate ……. (alama 2)

(b) Eleza matumizi mbalimbali ya 'ni' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Nendeni mkamwite Kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani

(c) Taja ala zinazotumika katika kutamka sauti zifuatazo

i)/dh/ ……

ii)/gh/ …….. (alama 2)

(d) Ainisha matumizi ya –ema katika sentensi ifuatayo (alama 3)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Mwanafunzi mwema ametunzwa vyema kwa wema wake

(e)Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)

"Atamkuta papa hapa akija kesho".Alisema.

(f) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi na kiambishi ngeli (alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(g) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa.

i) Tano ondoa tatu matokeo ni mbili (anza: Mbili……) (alama 1)

ii) Mwalimu huyu anafunza Kiswahili

(Maliza kwa kiashiria kisisitizi) (alama 1)

iii)Ng'ombe aliyekuwa nyuma ya ua alichechemea kwa vile aliumia ukwato wake.(andika kwa wingi) (alama 2)

(h) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno lifuatalo (alama 2)

Ndwele

(i) Ainisha sentensi hii (alama 3)

Aliyenichokoza

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(j) Geuza sentensi hizi ziwe katika kauli ya kutendewa (alama 4)

i) Muktubi amempa mwanafunzi jarida.

ii) Bate alivua samaki wengi.

(k) Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo (alama 4)

i) Uhusiano wa zaidi ya hayo

ii) Kuonyesha chanzo

(l) Changanua sentensi ifuatayo kwa vistari/vishale (alama 4)

Kandanda ni mchezo maarufu duniani

(m)Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Wanafunzi ambao waliokuwa wakarimu walimpenda Bi Keti

(n) Yakinisha sentensi hizi (alama 2)

i) Asingeenda safari asingepata ajali

ii)Usije

o) Andika kwa wastani (alama 2)

Magoma hayo yatachezewa mawanjani

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

4 ISIMU JAMII

"Bwana mdogo," alisema kwa sauti ya kite.

'Naam Doctor,' Nikajibu.

'Leo wasikiaje?'

'Nafeel poa'

'Unafanya kazi gani?'

'Nasukuma rukwama'

'Eeh! Bwana, kama watakwa kuishi,acha hiyo kazi ya suruba, unasikia?'

'Ndiyo Doctor"(kisha akanipimapima kwa kifaa alichokuwa nacho…..)

'Leo!' Aliniambia huku akisimama wima na kuchezeshachezesha kifaa chake mkononi,

"N'takuruhusu kwenda nyumbani.Wapaswa kupumzika kwa mwezi mzima pasi kufanya lolote zito."

'N`takupa vidonge vya kumeza.'

'Asante Doctor ,' Nikamshukuru.

Maswali

a) Mazungumzo haya yako katika rigista gani? (alama 1)

b) Taja lugha zilizotumika katika mazungumzo haya (alama 2)

c) Fafanua sifa za sajili hii (alama 3)

d) Eleza dhima za lugha ya Taifa (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

e)Taja na ueleze matatizo mawili yanayoikumba lugha ya Kiswahili. (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA IV

KISWAHILI 102/2

1. UFAHAMU

(a).Moto / uvumbuzi wa moto (alama 1)

(*Yasizidi maneno manne ikiwa methali*)

(b).-Akingojea kulungu kunaswa na mtego wake

- Ilikuwa mapema hakuona haja ya kwenda nyumbani na kurudi (alama 2)

(c) .mawe / jiwe vijiti / kijiti (alama 2)

(d).Athari za moto

Faida	Hasara
-kuunguza	-kuteketeza (kuweza vyote)
-kuoteka	- uharibifu mkubwa usipodhibitiwa
-kuchoma	- kujenga utabaka
- mwangaza nk	(zozote 2x1)

(e).Mashariti ya kuenea kwa moto:

-moto ulipatikana kwake tu

-uzimwe mara tu baada ya kutumiwa

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

-usiibiwe wala kufichwa (zozote 2x1=2)

(f).Faida zote za moto

-chakula cha bure

-utajiri au ubwanyenye (kufaidi bila kufanya kazi)

-kupata utukufu (zozote2x1=2)

(g).

i) Kioja – ajabu / shairi

ii) Wimbombo – kijiti mama kilichopekechwa na kuwaka moto

iii) Alikokuzira – alikokuchukia / dharau

iv) Meza kichaka – kuteketeza / kuunguza (4x1=4)

2. UFUPISHO

a)

- utando wa ubongo (meningitis) huzua hofu
- huathiri ngozi inayofunika ubongo na uti wa mgongo
- bakteria huwa hatari kuliko virusi kwa kusababisha meningitis
- wagonjwa wengi watibiwapo haraka hupona lakini wengine huachwa wakiwa bubu au vipovu na wengine hufariki
- ugonjwa huu hutokea bila kutarajiwa, aidha kwa ghafla
- ni vigumu kutenganisha dalili za ugonjwa huu na magonjwa mengine ya kawaida
- ripoti hii ni kwa mujibu wa wataalamu wa afya (Hoja 7x1 =7 mtiririko = 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

b) Dalili

- watoto hupatwa na homa, hutapika, kukataa kula na kulia kwa uchungu
- aidha kufura kichwa , kupumua kwa haraka, kutupatupa miguu na mwili kujikunyata
- watu wakubwa hupatwa na maumivu makali ya kichwa na shingo nzito
- wao hutapika na kukosa ufahamu
- aidha hupatwa na mikono na miguu baridi, maumivu ya misuli kwa damu kuwa na sumu

Hatua:

Mhasiriwa yeyote anayeshukiwa apelekwe hospitalini mara moja.

hoja 5 za dalili

hoja 1 ya hatua 6x1=6 1 mtiririko

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) i) neno li-ya

ii) mate ya –ya (2x1=2)

b) Nende<u>ni</u> – hali ya amri / rai

<u>ni</u> – kitenzi kishirikishi kipungufu

- kitenzi kishirikishi
- kitenzi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

niliyemwacha – nafsi / nafsi ya kwanza umoja

nafsi ya kwanza / nafsi ambata

maktabani - kielezi mahali (4x ½ =2)

c) i) /d h/ - meno na ulimi

ii) /gh/ - kaakaa laini na ulimi

d)mwema – kivumishi (v)

vyema - kielezi (E)

wema – nomino (N)

e) – Alisema angemkuta papo hapo ikiwa angeenda keshoye.

- Alisema angemkuta papo hapo angeenda keshoye / siku iliyofuata (4x ½ =2)

f) aliyetumwa

hajaipata karo (2x1=2)

g)i) –Mbili ni matokeo ya tano kuondoa tatu.

- Mbili ni matokea ya tatu kuondolewa kwa tano. (alama 1)

ii) Mwalimu anayefunza Kiswahili ni yuyu huyu. (alama 1)

iii) Ng'ombe waliokuwa nyuma ya nyua walichechemea kwa vile waliumia kwato zao.

(4x ½ =2)

h) ndwele – ugonjwa

- maradhi *kutambua –alama 1* *sentensi - alama 1*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

i) a-kiwakilishi nafsi cha tatu umoja

li- kiwakilishi cha wakati uliopita

ye- kirejeshi

ni- kitendewa / shamirisho / nafsi ya kwanza umoja

chokoza- shina / mzizi wa kitenzi

a – kimalizio

- kiishio
- hali ya kutenda (6x ½ =3)

j)i) Mwanafunzi amepewa jarida na muktubi.

ii) Samaki wengi walivuliwa na Bate. (2x1=)

k)i)Uhusiano zaidi ya hayo

-tena / pia / vilevile / aidha

ii) kuonyesha chanzo

tangu, toka. *kutaja 2x1=2* *kutunga 2x1=2* (alama 4)

l)Kandanda ni mchezo maarufu duniani.

S	KN + KT
KN	N
N	Kandanda
KT	T + N +V + E
T	ni
N	Mchezo
V	Maarufu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

E duniani (8x ½)

m)-ambao / waliokuwa

- karimu (2x1=2)

n) i) Angeenda ½

Angepata ½

ii) usije – njoo / uje (alama 2)

o) Ngoma hizo zitachezwa nyanjani

4. **ISIMU JAMII**

a) -Hospitali

- Zahanati (2x1=2)

b) - Kiingereza

-Kiswahili (2x1=2)

c)- maswali na majibu

-mahojiano

-maelezo

-ushauri / wosia / mawaidha

-shughuli (kupimapima)

-masharti

-usiri *(Hoja za mwanzo 3x1=3)* *(kutaja ½)* *(kufafanua / maelezo ½* *(6 x ½ =3)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

d)

-umoja na utangamano

-mawasiliano miongoni mwa wananchi

-hutambulisha utamanduni

-huziba mipaka ya kikabila

-hurahisisha utawala / uongozi

-huleta ajira (2x1=1) *(Hoja za mwanzo mbili)*

e) Matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili

-dhana ya sheng

-lugha ya kwanza

-kiingereza kupewa hadhi zaidi ya Kiswahili

-kiswahili kama lugha ya ujanja

-uhaba wa walimu *(Hoja za mwanzo mbili 2x1=2)*

KARATASI YA V

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

SWALI LA KWANZA –UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Watu husema mengi kuhusu maisha, Wengine husema mtu anapozaliwa hatima yake huwa imeshaamuliwa na Mwenyezi na hata afanye nini hakuna wa kubadilisha, yaani kama *majaaliwa* yake ni awe mwizi stadi katika *siku zake za halafu*, basi atakuwa mwizi stadi bila shaka; kama majaaliwa yake ni awe daktari maarufu, basi atakuwa daktari mashuhuri, na kadhalika, Watu kama hawa wana msimamo sawa na ule wa raia wa Uyunani (Ugiriki)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

wanaoamini kuwa maisha ya kila binadamu yana sehemu mbili kuu: sehemu mbaya na sehemu nzuri. Wayunani hawa w'anashikilia kuwa kila mtu lazima azionje sehemu zote mbili katika aushi yake na kwamba haiwezekani kuliepuka jambo hili. Watu hawa pia wanaamini kuwa miungu wao ndio wanaoamua maisha yao yatafuata mkondo gani. Yaani, wana imani kamili kwenye jaala eti kwa vile *wino wa Mungu haufutiki*.

Kwa bahati mbaya, humu nchini mwetu wapo watu ambao wanashiriki imani hiyo ya majaaliwa. Wao wanaamini kuwa wanapozaliwa, kazi yao kuu ni kuponda raha kwani hatima yao Mungu anaijua na hata wafanye nini hawawezi kuibadilisha. Kwa hivyo kazi yao hapa ni kukaa *sambejambe* na kuingojea hatima hiyo. Ukipiga alinacha utagundua kuwa asilimia kubwa ya watu wanaishi katika ufukara mkubwa lakini si kwa sababu hayo ndiyo majaaliwa yao kama wanavyodai, lakini ni kutokana na tabia ya kufanya *msirimbo miradi* yote iliyo mbele yao.

Maisha si majaaliwa. Hutegemea mipango na juhudi. Mtu asipojibidiisha na kupanga maisha yake vilivyo, basi bila shaka mambo *yatamwendea mvange* na ataishia kuishi maisha ya ufukara wa sina sinani. Ukitazama binadamu wengi katika nyanja mbalimbali, utaona kuwa hawana utaratibu imara wa kuendesha maisha yao. Chukua mfano wa vijana.Wao ndio waliokabiliwa vikali na tatizo hili. Wawapo shuleni, wengi wao hawana haja na elimu. Wanaamini kuwa shuleni ni pahali pa kuonjea utamu wa maisha huku wakingoja kubaleghe na kuoa au kuolewa. Wengi hujihusisha na vitendo vya ajabu kama kushiriki katika migomo. Sigara haziwatoki midomoni. Majira ya jioni hawapatikani tena shuleni kwani huwa wametorokea mijini na vitongojini kuponda raha. Dawa za kulevya nazo ndizo hizo. Wengine wanazielewa zote kwa majina hata wameshawahi kuonja kila sampuli ya dawa zenyewe. Si ajabu kuwa tayari baadhi yao ni wagonjwa wa ukosefu wa kinga mwilini. Wapo wale *mahiri* wa kufanya biashara yenyewe ya kusambaza dawa hizo za kulevya; walanguzi waliokubuhu hasa. Kuwepo kwao- shuleni hakuhusiani kwa vyovyote na elimu. La hasha. Ni mahali tu kwa kusukumia miradi yao hiyo. Wengine ni majambazi. Wao hushirikiana na wavunja sheria wengine kupora mali ya wenyewe bila ya mtu yeyote kuwashuku. Haya yote huweza kuonekana kama *yamepigwa chuku*. Lakini ukikumbuka hivi majuzi kifurushi kilichojaa bunduki kilipatikana chumbani mwa mwanafunzi mmoja chuoni, basi utaanza kuyaamini haya yote.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Wanafunzi wengine huifanya kazi yao kuu kuwa ile ya kuwahangaisha wenzao. Katika baadhi ya shule, wanafunzi hasa wa kidato cha pili hujihusisha na vitendo vya kuwadhulumu wenzao wa kidato cha kwanza. Wengine wamefika kiwango cha kuwatisha na hata kuwapiga walimu wao. Wawapo huko nyumbani huwa ni balaa tupu, Baadhi yao huvaa mavazi ya ajabu. Kina dada huvaa nguo fupi kiasi kwamba utadhani wako uchi. Ukiwauliza kisa na maana wanakujibu kuwa eti ndio.mtindo. Wengine huweka herini chungu nzima masikioni mwao na kujipaka rangi za kutisha midomoni. Wengine bila kusita hushirikiana kimwili na wavulana na hata wazee ambao huwafurahisha daima kwa *darahima* na zawadi kochokocho. Ugonjwa wa 'Ukimwi' si mgeni kwao. Sababu kuu ni kuwa wengine, hasa waliokulia mijini, wana mazoea ya kutembelea vilabu na kushiriki ulevi pamoja na ngono. Si ajabu kwamba baadhi yao *wameenda jongomeo* na wengine wako safarini kuelekea kuko huko. Wakikutana na kina dada watalii kutoka ng'ambo wanazuzuliwa na hizo ngozi zao nyeupe pepepe na kuapa kuwa nao pia ni lazima watakuwa kama wao. Wanafanya juu chini kutafuta ngwenje ili kujinunulia vipodozi aina aina vya kupaushia ngozi zao. Wasichana wengine hawasomi tena. Wametulia tuli kama maji mitungini humo majumbani wakiwanyonyesha wana wao waliopata kupitia harakati zao hizo.

Wavulana nao hawaachwi nyuma. Neno ‘nidhamu’ ni istilahi mpya kwao. Wao wanaishi leo, kesho itajililia. Wengine nywele wameziacha kuwa *matimtimu* utadhani ni wajukuu wa majemedari wa vita vya Mau Mau. Wamejitoboa mashimo chungu nzima masikioni ili wavae herini mbilimbili au tatutatu kulingana na mtindo uliopo. Wengine hata nywele wameonelea bora kuzisuka ili wafanane sawa bin sawa na akina dada. Na ili wasiachwe nyuma sana na kina dada hao, hawasahau kuvaa mikufu inayong'ara kuliko hiyo ya akina dada. Nayo mitindo ya nguo huzihangaisha akili zao saa ishirini na nne za kutwa. Macho na masikio yao hukaa chonjo kila dakika ili wafahamu ni mitindo gani mipya iliyoingia hasa kutoka ng'ambo kunakoishi wazungu wenyewe. Wengine nywele wameziweka 'kalikiti'. Suruali wanavaa zilizoganda mwilini utadhani zimewekwa gundi. Nao wengine wana mikururo ya marafiki wasichana. Ukiwauliza kisa na maana ya kutongoja hadi wakati ufike wanasema ndio mtindo. Ukiwauliza na 'Ukimwi je? *Wanakuchezesha kayamba* huku wakilumba kuwa Ukimwi ni porojo tupu; eti wamefanya vituko vyao miaka yote hiyo; inakuwaje *hawajaenda na ulele ngoma?*

Hata hivyo, kwa vile *unga wa manga si dawaya chongo*, baada ya pata shika zote hizo, kilichokuwa na mwanzo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

kinaanza kufikia hatima yake. Ukweli unaanza kuchukua mahali pake. Muda ambao wangetumia kujizatiti kwa minajili ya siku za baadaye wanashtukia ghafla kuwa tayari umeshawapa kisogo. Majuto na mikasa inawafuata unyo unyo.

Ni muhimu sana vijana kufungua macho yao ili kuona mwanga.Wanafaa kuelewa fika kuwa ujana ni moshi tu. Dakika hii upo, dakika nyingine ushatoweka. Mungu alipoamua kuwa kila binadamu ni lazima apitie ujanani alikuwa na sababu maalumu. Ujana ni kipindi cha maisha cha kujifunga masombo kwa majukumu ya baadaye. Ni kipindi cha kujitafutia maarifa tunu. Iwapo hali ni kinyume, basi mambo hayana budi kwenda mrama

Maswali

1. Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama 1)
2. **Eleza** msimamo wa watu wengi imani kwenye jaala. (alama 2)
3. **Taja** vitendo vyovyote vinne vinavyoonyesha upotovu miongoni mwa vijana. (alama 4)
4. Kutokana na taarifa; **eleza** jinsi vijana wanavyo ambukizwa ugonjwa wa ukimwi (alama 3)
5. Unadhani ni mambo yapi mengine yanachangia tabia potovu kati ya vijana? (alama 2)
6. **Toa** maana ya: (alama 3)
   (a) Kufanya msirimbo
   (b) Unga wa manga si dawa ya chongo
   (c) Kwenda mrama

MUHTASARI

Soma habari ifuatayo kasha ujibu maswali

Miaka mingi ya kutawaliwa na wakoloni iliwafanya wananchi wengi kupuuza umaarufu na uadilifu wa lugha ya kiswahili kama lugha ya taifa kwa manufaa ya kuarifiana habari mbalimbali kwa ufasaha na kuelewana vema. Wakoloni pia waliwashawishi wananchi waone kwamba lugha ya Kiswahili ni kwa ajili ya watu wale wasiokuwa na elimu na kwa wale ambao hawajastaarabika. Kwa wale ‘wenye’ elimu na wastaarabu’, wakoloni waliwashawishi kuamini kwamba lugha ya kigeni, yaani kiingereza, ndivyo hasa lugha inayofaa kwa kujieleza na kufahamisana habari.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Kutokana na vikwazo hivi si ajabu kuona hadi hivi sasa, mwananchi halisi akijitwaza kwamba hawezi kujieleza kwa ufasaha au kumpasha mwenzie habari kwa ukamilifu mpaka atumie lugha ya kingereza. Hata katika maofisi mengine ya serikali, hadi hii leo, japo imesha kupitishwa kisheria kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa, bado utawaona wanaona wananchi wengine wanapendelea kuzungumza kiingereza wao kwa wao, ili wajulikane kwamba wana kisomo na wamestaarabika.

Vikwazo vya namna hii vimewalemea wananchi vile vile kwa upande wa magazeti. Utaona mwanainchi ambaye anafahamu kiingereza kidogo sana, akijinunulia gazeti kubwa la kingereza na kuanza kuzurura nalo kutwa nzima bila kuambulia mengi ndani yake. Pia utawasikia wananchi wengi wakijidai kwamba hawataki kusoma magazeti ya Kiswahili kwa sababu inakuwa vigumu kwao kuelewa mambo yaliyomo kama vile ambavyo wangelielewa katika gazeti la kiingereza.

Mabeberu wamesha tugundua kwamba tunao upotofu wa aina hiyo, ndipo utaona mara nyingi wanawaletea wananchi magezeti mengi ya kiingereza, mengine yakiwa na nia ya kuwapotosha wakijua kwamba watayasoma tu, mradi yameandikwa kwa lugha la kiingereza.

Mara nyingi taifa fulani la kibeberu likitaka tuchukiane na taifa jingine fulani ambalo ni adui yake kisiasa au kiuchumi, taifa hilo la kibeberu linaandika habari za uchochezi kwenye magazeti yao ya lugha ya kiingereza, mambo kuhusu taifa lile adui yake (ambalo si adui yetu). Magazeti hayo huandikwa kwa lugha nadhifu ya Kiingereza na kuletewa wananchi hapa nchini. Maskini wananchi wengine waliotopea kwa kudhani kiingereza ndicho lugha nzuri ya kigazeti, wanayanunua mara moja na kuanza kuyasoma magazeti hayo, na pia kuwapa watoto wao wasome. Matokeo yake ni kwamba, bila kujitambua, wanajikuta wanafanya yale Mabeberu waliyotarajia wayafanye, yaani wanaanza kuchukiana bure na taifa lile ambalo ni adui wa Mabeberu hao, lakini si adui zetu.

Madhumuni ya kuandika habari kwenye magazeti, ni kutaka kuwafahamisha wasomaji mambo yaliyotokea au yatakayo tokea siku hata siku,kwa lugha inayofahamika na kueleweka kwa urahisi bila kumtatiza masomaji ikiwa basi ndiyo madhumuni, kuna haja gani kutumia lugha ya kigeni ili kuwaelezea wasomaji wako jambo ambalo wangaliweza kueleza kuelezwa kwa lugha yao wenyewe ambayo wanaielewa vyema. Mtu aelezewapo jambo lenyewe kutoka moyoni na akilini kwa njia adili ambayo anaifahamu vyema undani wake, huelezea jambo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

pia wasomaji wake wataielewa kwa ukamilifu. Kwa ujumla jambo ambalo mwandishi huyo ataliandika kwa lugha ambayo ni ya asili yake na ambayo anaielewa vyema, halitamtatiza msomaji wake ambaye pia anaielewa vyema lugha hiyo.

Maswali

(a) Fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 30-40) (alama 6)

Nakala chafu

Nakala safi

. **Taja** mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika aya ya nne hadi ya sita (Maneno 50-60) (alama 6)

Nakala chafu

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Weka nomino hizi katika ngeli lake. (alama 2)

(i) Mvule

Kipofu

(b) **Tunga** sentensi kuonyesha matumizi ya parandesi (alama 2)

(c) **Andika** sauti mbili zinazotamkiwa menoni (alama 2)

(d) **Changanua** sentensi ifuatayo kwa kutummia jedwali.

Mwanafunzi huyu mwerevu atapita mtihani vyema. (alama 4)

(e) **Andika** katika kauli ya kutendesheka. (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(a) Iga

(b) Vaa

(f) **Onyesha** aina ya vitenzi katika sentensi.

Wewe umewahi kufika shule ukiwa umechelewa? (alama 2)

(g) **Andika** kulingana na maagizo yaliyotolewa. (alama 2)

Jina langu ni maliki lakini huitwa mali kwa kifupi. (Anza kwa: Watu ----------)

(alama 2)

(h) Kwa kutunga sentensi **eleza** tofauti kati ya:

Sentensi ambatano na sentensi changamano

(i) **Onyesha** aina za virai katika sentensi (alama 2)

Gari lao lilianguka kando ya jengo.

(j) **Unda** vivumishi kutokana na vitenzi : (alama 2)

(i) Samehe

(ii) Kakamaa

(k) **Eleza** matumizi ya viambishi vilivyopigiwa kistari. (alama 3)

(i) <u>Ka</u>andika barua

(ii) Ni<u>ki</u>soma kwa bidii nitapita mtihani

(iii) Oliech <u>a</u>cheza mpira vizuri

(l) **Kanusha**.

(i) Wakimenyanamenyana (alama 1)

Ningefika mapema ningewahi basi hilo (alama 1)

(m) **Onyesha** aina za mofimu zilizopigiwa kistari. (alama 2)

Alisita alipofika chumba cha <u>sita</u>

(n) **Tunga** sentensi kubainisha: (alama 2)

(i) Inchi

(ii) Nchi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(o) **Sahihisha** sentensi ifuatayo.

Mkutano uliyohairishwa juma lililopita utafanywa leo (alama 2)

(p) **Andika** katika usemi wa taarifa:

"Nikifaulu nitamshukuru sana Mungu pamoja na wazazi wangu." Mungai alisema. (alama 3)

(q) **Andika** katika wingi:

Kuku wa jirani kijijini mwetu aliangua kifaranga aliyelemaa. (alama 2)

Isimu jamii (alama 10)

Taja na ueleze njia tano zinazochongia maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini.

(alama 10)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA V

KISWAHILI 102/2

Ufahamu

1. Amkeni vijana / vijana wa leo / maisha ni mapambano maisha si majaaliwa n.k. (1x1 =1)
2. – Maisha yamepangwa na mwenyezi Mungu na binadamu hawezi kubadilisha.
   - Maisha yana pande mbili nzuri na mbaya na ni lazima uyapitie
   - Yana utamu na uchungu, raha na dhiki zake (2x1=2)
3.

- ❖ Kushiriki katika migomo
- ❖ Kuvuta sigara
- ❖ Mihandarati / ulevi
- ❖ Ngono
- ❖ Usambazaji wa dawa za kulevya (ulanguzi)
- ❖ Kutotilia elimu maanani
- ❖ Ujambazi
- ❖ Kuwadhulumu wenzao
- ❖ Mavazi ya ajabu / mitindo ya nywele
- ❖ Kuiga wazungu
- ❖ Athari za makundi na rika (peer pressure) (1x4 = 4)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

4.

- Kushiriki ngono ili wapate derahima
- Kushiriki ulevi
- Kutembea vilabu na mafuska yenye,ukahaba mwingi (1x3 =3)

5.

- Vyombo vya habari
- Kuiga mitindo ya kigeni
- Ukosefu wa malezi na maadili
- Ukosefu wa vielezo katika jamii n.k.
- Vitabu na majarida yenye maelezo na picha chafu (1x2=2)

6.

(i) Kufanya msirimbo – usira / mzaha / puuza/ dharau n.k.

(ii) Unga wa manga si dawa ya chongo – kutenda yasiyofaa huwatumbukiza katika matatizo / kuponda raha sio suluhisho bali ni karaha / kulaumu ugonjwa bila kuchukua tiba si suluhisho (1x3=3)

(iii) Kwenda mnama / haribika / vurugika nk

(a)

UFUPISHO

- Miaka mingi ya kutawaliwa kumeifanya lugha ya Kiswahili kupuuzwa.
- Wakoloni waliwashawishi waafrika waione ni lugha ya watu wajinga
- Waliwashawishi waafrika kukitukuza kiingereza
- Athari hii imewafanya waafrika kushindwa kuasiliana kwa lugha ya Kiswahili
- Ingawa ni lugha ya taifa wengi ofisini wanapendelea kutumia kiingereza
- Kiingereza hutumiwa kama ishara ya ustaarabu hoja zozote

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- ❖ Kukolezwa kasumba ya lugha za kigeni

(b)

- ❖ watu hununua magazeti ambayo hawayaelewi
- ❖ hudai Kiswahili ni lugha ngumu kusomwa magazetini kuliko kiingereza
- ❖ Ndio maana kuna magazeti mengi ya kiingereza
- ❖ Huyasoma kwa kuwa ni ya kiingereza
- ❖ Uchochezi wa kibeberu huendelezwa katika magazeti ya kiingereza humu nchini
- ❖ Matokeo yake ni chuki kati ya mataifa yasiyokuwa na uhasama. 1 x 6 = 6

Taz: mtahiniwa apewe alama 3 za mtiririko kutegemea umahiri wake

: Pia hati safi inayosomeka ijumlishwe kati ya hizo maki tatu.

MATUMIZI YA LUGHA

(a)

(i) Mvule – u - i (Yaani Mvule huu, mivule hii)

(ii) Kipofu - a – wa (yaani kipofuala – vipofu wala) 1x2=2

(b) Parandesi / mabano ( ) Braketi matumizi yake katika sentensi

- ❖ Ufafanuzi k.m. Wema hauozi (hisani haiozi)
- ❖ Huonyesha maneno yasiyokuwa ya lazima K.m shule ya Alliance (iliyoongoza katika mtihani wa KCSE) ilituzwa.
- ❖ Kuzingira herufi au nambari k.m (1) (2) 1x2=2

(c) Sauti za menoni /th/ /dh/ 1x2=2

(d) Uchanganuzi

S✓				
KN✓			KT✓	
N	V	V	T	KN

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

			N	E
Mwanafunzi	huyu mwerevu	atapita	mtihani	vyema

(e) Iga - igizika
Vaa - valishika 1x2=2

(f) Wewe umewahi kufika shuleni ukiwa umechelewa?
Ts T Ts T ½ x4 =2

Ts = vitenzi visaidizi T= (vitenzi vikuu)

(g) Watu huniita mali kwa kifupi / ingawa /jina langu ni maliki 2 x1= 2

(h) Sentensi ambatano huwa ni sentensi mbili au zaidi zilizounganishwa kwa kiunganishi.
Sentensi changamano / changamani hujumuisha vishazi vitegemezi. Huwa na kishazi kitegemezi ambacho hutegemea kishazi kingine huru kwa kutumia viambishi kama –po- -ki- -nge- na –ngali-
(2x2 =4)

(i) Gari lao lilinguka kando ya jengo
Gari lao – kirai nomino
Kando ya jengo – kirai kihusishi (1x2=2)

(j) Samehe – samehevu , usamehevu
Kakamaa- kakamavu , ukakamavu (1x2=2)

(k)
(i) Kaandike barua – amrisha
(ii) Nikisoma kwa bidii nitapita mtihani – masharti / lazima / shuruti
(iii) Oliech acheza mpira vizuri – Wakati usiodhihirika. (1x3=3)

(l)
(i) Wasipomenyanamenyana

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(ii) Nisingefika mapema nisingewahi basi hilo. 1 x 2 = 2

(m) Alisita – mofimu tegemezi

Sita – mofimu huru (1x2=2)

(n) Inchi – kipimo cha urefu

Nchi –sehemu ya ardhi (1 x 2 = 2)

Mkutano ulioahirishwa juma lililopita utafanywa leo. (2 x1=2)

(o) Mungai alisema kama angefaulu angemshukuru sana Mungu pamoja na wazazi wake.

(3x1 =3)

(p) Kuku wa majirani vijijini mwetu, waliangua vifaranga waliolemaa. (2x1=2)

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Njia zinazochangia maenezi ya Kiswahili.

- ❖ Dini
- ❖ Biashara
- ❖ Shule inatahiniwa viwango vyote
- ❖ Vyombo vya habari – magazeti / runinga / filamu
- ❖ Ndoa baina ya watu wa jamii tofauti
- ❖ Malezi ya kisasa
- ❖ Lugha ya taifa / rasmi

(zozote tano na maelezo sahihi 2x5=10)

- ❖ Vitabu vya riwaya / ushairi/ tamthilia vya waandishi mbalimabali
- ❖ Tamasha za muziki na maigizo
- ❖ Mijadala na hotuba mbalimbali redioni na katika mabaraza.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA VI

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

1. UFAHAMU.

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali.

Turipoguria nyumba mpya, tulimkuta paka. Rehema hakuingiwa na kicho maana namjua itikadi zake. Mara angesema kuwa huyo si paka ni pepo na kuwa nyumba ile halikaliki. Paka yule mara akataka kuitamalaki nyumba, kuiimgia mapana na marefu. Mimi tabia yangu simpendi paka. Kwa hakika sipendi kufuga fuga vinyama, hunitia dhiki sana nami huona navikutisha mashaka tu. Zaidi ya yote, paka hunichemuza.

Lakini tulipoingia tu akafanya mazoea na Rehema akawa kila aingiapo amwandama unyounyo naye akawa ni mzungumzi wake mkubwa. Utamsikia Rehema asema naye kama asemaye na mtu.” Paka wewe u roho mno, uonacho wataka? Siku moja utakuja niangusha huishi kuniingia maguuni?”

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Mimi huku nakereka. Kila nikimwambia Rehema amtupe huniambia; “leo nitamshika”. Nikirudi yu papo. Hata nilipomsikia akinung’unika kuwa, “Mtu humchukuaje kiumbe akaenda akamtupa bure?”, nikajua hana azma ya kumtoa mle nyumbani.

Hayo yasitoshe, kila usiku takriban alikuwa akija na genge wakatuhanikiza kwa vishindo vyao huko darini wakikimbizana na kupapurana tukawa nyumba nzima hatupati usono. ‘ mapenzi ya kipaka yana vituko!’ Hata Rehema akawa anamwambia: “paka wewe nawe watia aibu. Huna haya hata kidogo. Uingie kwa watu, uwalie vyao, uwatilie na wanaume pia! Basi hata humstahi mwenye nyumba! Ndipo mwenyewe akawa hana jicho la kukushuhudia.”

Ilikuwa sharuti nitafute mwenyewe tadubiri ya kumtolea mbali nduli yule. Kweli alikuwa nduli kwangu; mafua yakawa hayaniishi na pia zikawa zaingia ishara za pumu. Nikafikiri nimwambie kuwa nimekwenda kutazamia nikaambiwa kuwa yule ni shetani amekuja kutudhuru kwa kujitia urafiki.

Nikaona hivi sivyo. Kuchezacheza na itikadi na hofu za mtu kwaweza kuleta hasara usiyoikadiria. Nikawaza. Ikanijia fikira kuwa paka huyu lazima ni wa watu waliokuwa wakikaa humu kabla hatujahamia sisi. Akafanya mazoea sana humu ama akaachwa papa hapa au akachukuliwa akakimbia. Nikawaambia wenyewe. Ikasadifu kuwa nilivyofikiri ndivyo ilivyokuwa. Wenyewe walikuwa washakata tamaa kuwa watampata tena paka wao.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

a) Kwa nini msimulizi hakumpenda paka? (alama 4)

b) Eleza njia ambazo msimulizi alifikiri kuzitumia ili kumwondoa paka kutoka mle nyumbani. (alama 3)

c) Fafanua hatima ya kila mojawapo ya njia ulizotaja katika swali la (b) hapo juu. (alama 3)

d) "Rehema ni mtu mwenye itikadi"thibitisha kwa mujibu wa taarifa. (alama 2)

e) Ni nini kinachoonyesha kuwa rehema alimpenda paka huyo? (alama 1)

f) Eleza maana ya mafungu haya kama yalivyotumiwa taarifani. (alama 2)

(i) Hakuingiwa na kicho.

(ii) Tadibiri ya kumtolea mbali.

1. MUHTASARI

Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu huathirika na biashara ya kimataifa. Biashara hiyo inaweza kuwa inafanywa kwa uagizaji ama uuzaji wa bidhaa nchi nyingine.

Biashara ya kimataifa ina umuhimu mkubwa. Kwanza, inaiwezesha nchi kupata bidhaa ambazo haizitengenezi mbali na kusaidia kuwepo uhusiano kati ya nchi mbalimbali. Uhusiano huu huiwezesha nchi kupata bidhaa kwa bei rahisi kuliko ambavyo ingekuwa kama zingetengenezawa kwao, hasa wakati nchi inayohusika haina malighafi yanaohusika katika utengenezaji wa bidhaa hizo. Pia, husaidia wakati

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

nchi imekumbwa na dharura au majanga kwani itaauniwa na nchi nyingine ingawa hali kama hii haihakikishwi. Ushirikiano huu vilevile huchochea upatikanaji wa nafasi za kazi kwa wengi.

Kwa sababu za kushughulikia utengezaji wa bidhaa na utoaji huduma nyingine kutakana na uzoefu wa muda mrefu na kuwepo raslimali, nchi huwa na uzoefu fulani. Ni kwa sababu hii ndio nchi inaiwezesha kupata pesa za kigeni na kuuza bidhaa za ziada.

Hata hivyo, kuna matatizo yanayozikumba nchi za kiafrika katika biashara hii, yanayotokana na ukosefu wa usawa baina ya nchi zinazoshiriki biashara. Kwanza, biashara ya aina hii hutatiza viwanda vichanga katika nchi zinazoendelea kwa ushindani usio sawa. Ajabu ni kwamba nchi ziliozoendelea zimetumia biashara hii ‘kutupa’bidhaa za hali ya chini ama zenye athari kwa hali za kijamii. Urafiki haukosi. Ikiwa nchi inategemea uagizaji wa bidhaa, haitaweza kuikosa ama kuhitilafiana na nchi ambayo inaitegemea, hivyo kuathiri uhuru wa nchi kama hiyo.

Hata hivyo, nchi mbalimbali zimeweka mikakata ya kulinda viwanda vichanga kutokana na athari za biashara kama hii. Baadhi ya nchi zimeweka ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kwa wasio washirika wao kibiashara. Licha ya hayo, baadhi ya bidhaa zinazonuiwa kwa nje kwa matumizi ya kielimu, urafiti wa kisayansi na bidhaa za maonyesho huagizwa bila ushuru huo. Wakati mwingine ni Banki kuu ndiyo hutoa leseni kwa niaba ya serikali kama njia ya kudhibiti bidhaa kutoka nje. Njia nyingine za kuvisaidia viwanda nchini kuuza bidhaa kwa ya chini ya kuvipunguzia ushuru, usafirishaji nafuu na kuvipa mikopo.

Serikali nyingine huhakikisha kuwa ni bidhaa kiasi Fulani tu ambazo zinaweza kuagizwa kwa kipindi Fulani. Kwa mfano, kuna idadi fulani ya magari kutoka nje yanayoweza kuagizwa kuja Kenya kwa mwaka mmoja. Hata hivyo, wakati mwingine, serikali husitisha uagizaji wa bidhaa kama vile dawa, sinema, maandishi ya kisiasa na vitabu kutokanje; bidhaa ambazo zinachukuliwa kuwa hatari kwa nchi.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

a) Fafanua mambo yote muhimu yanayozungumziwa katika aya za kwa kwanza tatu

(maneno 40-50)

Matayarisho (alama 8, 1 ya utiririko)

Jibu

b) Fupisha aya za mwisho mbili bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi.

(maneno 45)

(alama 7, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Jibu.

3 **MATUMIZI YA LUGHA**

a) **Kamilisha kwa mnyambuliko sahihi**. (alama 1)

kitoto kichanga kilipo…….. kilichangamka sana (oga).

b) Majina mengi katika ngeli ya U-ZI huchukua kiambishi U katika umoja lakini viambishi tofauti katika wingi.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Andika majina matano ukionyesha viambishi hivyo tofauti katika umoja na wingi. (alama 2 ½)

c) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo: (alama 2)

Chakula chote kitaharibika.

Chakula chochote kitaharibika.

d) Zifuatazo ni amri gani za konsonanti na hutamkiwa mahali gani? (alama 2)

(i) /h/

(ii) /r/

e) Sahihisha sentensi: (alama 2)

Mama mwenye alikufa amezikwa katika kaburini.

f) Ainisha sentensi ifutayo kwa mfumo wa mstari (alama 3 ½)

Ng'ombe waliovamia shamba letu wamesababisha uharibifu mkubwa.

g) Sentensi hizi ni za aina gani? (alama 2)

(i) Mkulima aliyekata rufani atasaidiwa kesho.

(ii) Walimu na wazazi wanatengeneza bweni.

h) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa. (alama 2)

(i) Ngome ya wanajeshi ilifanyiwa ukarabati.(Andika katika hali ya mazoea).

(ii) Gali hili lapendeza. (tumia kivumishi kisisitizi).

i) Bainisha virai nomino, virai vivumishi kisisifizi katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Yule mwalimu mwenye ndevu amewasili ukumbini sasa hivi.

j) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 1)

Wao wangeniazima kalamu tungemaliza kazi kwa wakati.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

k) Tunga sentensi kwa kutumia ‘msemo kuwa’ mauza’ili kutoa maana sahihi. (alama 2)

l) Kamilisha methali ifuatayo (alama 1)

Kuku akiacha wana……

m) Andika kinyume cha: (alama 2)

Benati yule alifanya kazi polepole.

n) Tofautisha vitate vifuatavyo kwa kuvitungia sentensi moja (alama 2)

Kucha na kuja.

o) Andika udogo na ukubwa wa neno; Mwana. (alama 2)

p) Andika visawe vya maneno haya: (alama 2)

(i) Mwehu-

(ii) Mahuluku-

q) Bainisha shamirisho kipozi na shamisisho kitondo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Onyango alimnunulia simu mpenzi wake.

r) Andika katika msemo halisi. (alama 2)

Maina alisema kwamba njiani kulikuwa kumenyesha sana ndio sababu walichelewa.

s) Eleza matumizi ya vile katika sentensi hii: (alama 1)

Vile vile seremala alitengeneza meza.

t)(i) Jumla ya ishirini huitwa…….. (alama 1)

(ii) Jumla ya miaka kumi huitwa …….. (alama 1)

u) Chea cha mtu afanyaye kazi katika maktaba huitwa…….. (alama 1)

4 **ISIMUJAMII**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Bwana mwenyezi, muumba wa ardhi na mbingu, twaja mbele yako asubuhi hii kukuomba uendelee kutulinda na kutumiminia kila kilicho chema. Bariki ibada ya leo na sheshe ya sindikiza ya kina mama tutakayokuwa nayo alasiri. Ninaomba haya machache kwa jina la yesu Kristo mkombozi wetu, Amina.

(a) Taja muktadha wa makala haya. (alama 2)

(b) Taja sifa zozote tatu za sajili hii zinazojitokeza katika makala haya. (alama 3)

(c) Taja sifa zingine za lugha ambazo hazikuhusishwa katika makala haya kwa mujibu wa sajili hii. (alama 5)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA VI

KISWAHILI 102/2

1 a) - Paka humchemuza
- Alikuja na genge usiku na kuwakosesha usingizi(milio yake)
- Hana aibu / haya.
- Aliwalia vyao.
- Alimletea mafuta na pumu (nduli) zozote 4x1=4

b) - Alimwambia Rehema amtupe.
- Alifikiri kumhadaa kuwa alienda kutazamia akaambiwa kuwa yule ni adui aliyejitia urafiki ili awadhuru.
- Aliamua kuwaambia 'wenyewe' walioishi kule kabla ya wao. 3x1=3

c) - Rehema alikataa kumtupa kwa kutoona ubaya wake.
- Aliona kuwa kuchezacheza na itikadi na hofu za mtu kungeleta hasara isiyokadiriwa.
- Ilisadifu akawapata wenyewe 3x1=3

d) - Msimulizi adai kuwa alimjua kuwa na itikadi.
- Hakuingiwa na kicho/ hofu alipomkuta paka mle nyumbani.
- "Mara angesema kuwa paka yule ni pepo na nyumba ile haikaliki.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Zozote

2x1=2

e) - Alikuwa akimwandama unyounyo
- Alikuwa mzungumzi wake mkubwa.
- Hakuona haja / sababu ya kumfukuza hoja yoyote

1x1=1

f) (i) Hakuogopa/ hakushtuka.
(ii) Azma / mpango wa kumwondoa pale. 2 x 1 = 2

2 a) (i) Biashara ya kimataifa haisadii nchi zinazoendelea.
(ii) Inawezesha nchi kupata bidhaa isizotengeneza.
(iii) Huleta uhusiano mzuri kati ya nchi mbalimbali.
(iv) Husaidia wakati wa dharura / majanga.
(v) Hotoa nafasi za kazi kwa wengi.
(vi) Huimarisha ubora wa bidhaa kutokana na uzoefu.
(vii) Huwezesha nchi kupata fedha za kigeni na kuuza bidhaa za ziada.

7x1=7

b) (i) Nchi zimeweka mikakati ya kulinda viwanda vichanga.
(ii) Kuwekwa kwa ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa.
(iii) Kupunguzia viwanda vyao ushuru.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(iv) Kuvipa viwanda vyao mikopo ya upanuzi wa maendeleo.

(v) Kuhakikisha usafirishaji nafuu kwa viwanda vyao

(vi) Kuweka viwango vya bidhaa zinazoweza kuagizwa kutoka nje kwa kipindi fulani. 6x1=6

3 a) Kilipoogeshwa

b) (i) Ukuta-kuta/ukucha-kucha/ukuni-kuni

(ii) Ubao-mbao/ubavu-mbavu/ubawa-mbawa

(iii) Ulimi-ndimi

(iv) Wimbo-Nyimbo/waya-nyaya/ wakati-nyakati/waraka-nyaraka

(v) Ufito-fito

(vi) Uso-nyuso/uzi-nyuzi zozote 5x ½ =2 ½

c) Chote – ujumla wa vitu bila ya kubaki (kila kimoja) 2x1=2

Chochote bila kubagua / uchaguzi

d) (h) - kikwamizo-koromeo

(r) - kimadende-ufizi 4x ½ =2

e) Mama <u>ambaye alikufa</u> amezikwa <u>kaburini</u> au

Mama <u>aliyekufa</u> amezikwa <u>katika kaburi.</u> 2 x 1 = 2

f) (KN)N- Ngo'mbe

(K.T)T- Waliovamia

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

N - shamba
V - Letu
(KT)T - Wamesababisha
(KN)N - Uharibifu
V - Mkubwa

g) (i) Changamano
(ii) Sahili 2 x 1 = 2

h) Ngome ya wanajeshi hufanyiwa ukarabati. 1 x 2 = 2

i) Yule mwalimu - virai nomino
Mwenye ndevu - virai vivumishi
Sasa hivi - virai vielezi. 3 x 1 = 3

j) - Wasingeniazima
- Tusingemaliza 2 x ½ = 1

k) Kowa manza - patwa na makosa 1 x 2 = 2

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

l) Kuku akiacha wana ana mayai tumboni 1 x 1 = 1

m) Benati - Mvulana
Polepole- Chapuchapu/ haraka 2 x 1 = 2
-

n) Kucha - kipande kigumu mfano wa pembe kinachoota kwenye kidole cha mtu
(mnyama au ndege)/ Heshimu / Pambazuka.
Kuja – tamko la kumwita mtu

o)

Udogo	Ukubwa	
kijana	jana	2 x 1 = 2

p)

Mwehu	-	kichaa/ mwendawazimu	
Mahuluku	-	mtu/binadamu/mja/kiumbe/insi	2 x 1 = 2

q)

Kipozi	-	Simu	
Kitondo	-	Mpenzi wake.	2 x 1 = 2

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

r) **M**aria alisema,"**N**jiani kulikuwa kumenyesha sana ndio sababu **t**ulichelewa."

4 x ½ = 2

s) Pia 1 x 1= 1

t) (i) Korija 2 x 1 = 2

(ii) Mwongo

u) Uktubi 1 x 1 = 1

4 **ISIMUJAMII**

a) Muktadha wa kidini/ maabadini/ kanisani
Ni maombi kwa mwenyezi Mungu yanayotolewa na muumini.

b) - Msamiati teule wa dini .k.v. Bwana Mwenyezi, bariki ibada ya leo, kwa jina la Yesu Kristo.n.k.
- Lugha ya unyenyekevu/ upole k.v. twaja mbele zako asubuhi…..
- Lugha ya heshima na adabu bila kutumia misimu k.v. tunaomba,

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Ni mazungumzo ya mtu mmoja yakielekezwa kwa muumba. Zozote 3x1=3

c)
- Kuna kurejelea sura au aya za maandishi matakatifu k.v. Biblia
- Lugha rahisi / ya kueleweka hutumiwa.
- Mkalimani huhitajika ili kuweka wazi kinachosemwa.
- Lugha huhusisha kubadilikabadilika kwa sauti kutegemea madhumuni.
- Kuzungumza kwa pamoja hutokea hasa katika maombi.
- Lugha ya ishara hasa za mikono hutumika
- Lugha ya kishairi ama kifasihi hutumika
- Lugha isiyo chuku / misimu n.k. zozote 5x1=5

KARATASI YA VII

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

1. **UFAHAMU**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Mzawa alikuwa mziwanda miongoni mwa ndugu zake wanne. Alipopigwa darubini, alionekana kuwa mwanagenzi ambaye falau angemakinika angefikia upeo wa ufanisi masomoni kwa kuwa na vipawa adimu vilivyofaa kuchochewa, kufukutwa, kurandiwa na kapigwa msasa. Nia ingekuwepo njia ingepatikana. Wala hakuwa peke yake. Kulikuwa na wengi kama yeye. Na kisiki kilichomkingamia kilikuwa kipi? Kisiki kilichokuwepo kilikuwa kwamba licha ya kuwa katika kidato cha tatu na mwenye umri wa miaka yapata kumi na sita, alikuwa mfano wa ajabu ya shingo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

kukataa kulala chini, hakukomaa. Na mtu ataitwa mtu vipi bila kukomaa? Wenzake darasani walimwita ‘toto kuu’ kwa kuwa japo alionekana katutumka, tena mlingoti, alidinda kukaramka. Nao utu mzima hufunzwa katika taasisi gani? Jawabu la swali hili lingalipatikana lingalimfaa sana Mzawa.

Na usidhani wasiokomaa ni waziwando tu, hata vifunguamimba na wanuna wao wote waweza kukomaa kutegemea misukumo, ari na mazingira yaliyo karibu nao. Mtoto azaliwapo, bongo lake huwa ombwe tupu na chochote kiingiacho humo huwa kama kinachoandikwa kwa wino usiofutika, hunata kama gundi. Ukomavu huanzia hapa na mzazi akifanya waa katika maneno na vitendo afanyavyo kwa mtoto, huenda akachangia kwa kutokomaa kwake.

Mzawa hakuwa na umbu. Hii ilionyesha kuwa, kwa kuwa wazaziwe walikuwa wamejikopoa wana wanne wa jinsia moja, walimngojea mwana wa jinsia tofauti kwa hamu na ghamu. Si ajabu kuwa pindi alipozaliwa waliamua kufikisha uzazi hatima yake baada ya kupata walichokikamia. Msisimko uliowapata wazazi wa Mzawa ndio uliowapeleka kumtendekeza. Na ni kwa nini wazazi wengi huwa hawatosheki kamwe kwa kuwapata watoto wa jinsia moja tu? Si ajabu kuwaona wengine wakijifungua hata zaidi ya wana kumi, tena katika karne hii ya upangaji uzazi, lengo likiwa kusaka jinsia wasiyojaliwa kuipata. Sijui ni nani atakayeuganga ukongo huu.

Mama Mzawa alipofunga mkaja, walisitisha shughuli zao zote, wakawa wanasherehekea kwa vigelegele, wakikipakata kitoto chao kwa zamu zilizorembeshwa kwa mashairi ya sifa za utanashati wa mwanao kwa mahadhi mbalimbali yaliyotiwa udamisi ajabu. Msisimko kama huu lazima uwepo huwatokea wampatao mwanao wa kwanza na hasa waliolimatia kujikopoa, hivyo baba mtu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

akaamua hataitwa tena jongoo asiyeukwea mtungi na mama hataitwa tasa. Hili huzua hatari ya kumdekeza mwana, naye atadeka milele kama huyu Mzawa.

Wazazi wa Mzawa hawakumkomaza. Kila kuchao walimwita ‘mtoto’, naye akawa mtoto wa kweli hata akafikia kidato cha tatu. Yasemwa kuwa Mzawa alilikamata ziwa la mamaye hata akafikia darasa la tano. Haikuwa ajabu kumpata mamake akimsubiri njiani eti waziwa yanamwasha, naye mwanawe amekishika kilembe kadamnasi ya watu huko njiani, huku amepakatwa kiweoni. Kisha akishakinai kuama, angeelekwa kwa ubeleko hadi nyumbani alikomkuta babaye aliyemngojea kwa ilhamu na kwa nyimbo za kumuongoa hadi alale.

Hadi afike hapo alipokuwa sasa, Mzawa hakujua hata kunawa uso. Daima alioshwa na mvyele wake bila hata kuona soni kwa kuwa aliamini kuwa bado ni mtoto- mfikirie mtu aliyevunja ungo akioshwa na mamaye! Izara yafaa kumkumba, ila Mzawa alinyimwa soni. Ama ndiye aliyezua maneno, “waso haya wana mji wao?” Kama walisema avuliwaye nguo huchutama, ikawaje hata Mzawa avuliwa nguo na hata kukoshwa? Jitihada za nduguze kumkebehi na kumwambia ajitegemee na zile za majirani kuwasuta wazazi wa Mzawa ziliambulia patupu.

Hii sasa ni shule ya sita aliyosomea. Mzawa tangu aingize mguu wake katika shule ya upili. Kila aingiayo haimweki. Mara atasingizia kuwakosa wazazi wake, mara atalia eti chakula ni kigumu, atasema aona baridi akilala peke yake kwa kuzoea kulala mbavuni mwa wazae wake, homa ikimpata hulia kuwa hatunzwi, mwili haogi na hata anaposhikiwa shokoa na wenzake hajui kunawa hata uso! Huyaacha matongo yakiwamulika watu. Naye hunuka fee! Mahali alalamo ungedhani ni makao ya beberu kwa mnuko. Harufu aliyotoa viatuni mwake ingesababisha pua kung’oka na mapafu kurudi. Alimradi Mzawa au “toto kuu,” kama alivyobatizwa, alikuwa zaidi ya mtoto. Na

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ingawa ni mapema sana huyawaza haya, je, Mzawa atakomaa, atengenee, apate ajira, apate mbawaze arukie au atakuwa kinda milele? Atapata kufu yake hatimaye?
Wako wapi hawa vifungamimba, wanuna au waziwanda waliokomaa wawakomaze wawakomaze wasiokomaa? Ama wewe usomaye wasubiri kwenda likizoni kupakatwa na wazazio? Tabia zisizoafiki umri wa mtu huongonga, na wenye hekima walitufaa waliposema, "Mtoto akinyea kiweo hakikatwi," tutakiosha 'kiweo' chenyewe mtoto aadilishwe aadilike, aadibishwe aadibike.

MASWALI

(a) **Yape** makala haya anwani mwafaka. (alama 1)

(b) **Eleza** vile wazazi wa mzawa walivyochangia katika tabia yake (alama 3)

(c) **Kwa nini** shule mbalimbali hazikuweza kumweka Mzawa? (alama 4)

(d) Kwa kuitolea mifano, **taja aina nne** ya tamathali za usemi zilizotumika katika taarifa uliyoisoma. (alama 4)

(e) **Eleza** maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala. (alama 3)

(i) Mziwanda –

(ii) Kukaramuka –

(iii) Waa-

2. **UFUPISHO**

Soma makala yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu; kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa idhini maalum ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama. Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizo nazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati ipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari; amefika mwezini; amevumbua uyoka; amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambacho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri dunia kwa kila lilo jema kwa siku sita mtawalia na kumpa binadamu mazingira murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri, akamwambia binadamu, “haya, twende kazi.”

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji – taka ovyo hadi mitoni, maziwa na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambayo ni urithi aliopewa na muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya ‘maendeleo’ yake. Moshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozoni ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya asidi inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa ‘tsunami’ bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi. Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe.

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengine kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya basafu!

Maswali

(a) Bila kupoteza maana asilia, **fupisha** aya ya kwanza na ya pili. (maneno 50-60).
(alama 5 – alama1 ya Mtiririko).

Matayarisho

Jibu

(b) **Eleza** mambo muhimu yaliyoshughulikiwa na mwandishi katika aya nne za mwisho.
(maneno 90-100) (alama 8- alama 1ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

3. Matumizi ya lugha

(a) **Akifisha** kifungu kifuatacho

mimi naona ni kazi ngumu nilimjibu si kazi ngumu ni mboga tu aliniambia huku akiniangalia kwa jicho la kunirai (alama 4)

(b) **Sahihisha** sentensi zifuatazo:

(i) Kikombe ya mwalimu yetu ambacho kilichovunjika kilikuwa ndani ya kabatini. (alama 2)

(ii) Mgeni alikodisha chumba cha kulala baada ya kuburudika na muziki. (alama 1)

(c) **Eleza** maana ya sentensi hizi:

(i) Alitukimbia kabisa. (alama 1)

(ii) Alitukimbilia kabisa (alama 1)

(d) **Andika** katika usemi wa taarifa.

"Rejelea maelezo katika kitabu ili kuhakiki majibu yako." Mwalimu alimwambia mwanafunzi. (alama 2)

(e) **Tumia** nomino zifuatazo katika sentensi kama vivumishi.

(i) mlevi (alama 2)

(ii) huru (alama 2)

(f) **Onyesha** fungu nomino na fungu tenzi katika sentensi ifuatayo:

Anapenda kusoma gazeti lenye maswala ya kijamii. (alama 2)

(g) Majina yafuatayo hupatikana katika ngeli gani?

(i) Chumvi (alama 1)

(ii) Nyama (alama 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(h) **Onyesha** silabi inayawekwa shadda kwenye maneno haya:

(i) Karatasi (alama 1)

(ii) Samahani (alama 1)

(i) **Onyesha** chagizo na yambwa katika sentensi ifuatayo:

Mwanafunzi amesoma kitabu vizuri sana. (alama 1)

(j) **Tumia** –amba katika sentensi hii:

Ua limealo huwa limetiwa mbolea. (alama 1)

(k) **Andika** sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:

(i) Barmasai huzungumza kilatini vizuri sana.(Tumia wakati usiodhihirika). (alama 1)

(ii) Mtoto huyu hula chakula kingi sana. (Kanusha katika hali ya ukubwa) (alama 1)

(l) **Unda** nomino kutokana na vitenzi hivi:

(i) Hakiki (alama 1)

(ii) Subiri (alama 1)

(iii) Sajili (alama 1)

(m) **Andika** sentensi ifuatayo katika wingi hali ya kukubali

Mgonjwa hasemi hajanywa dawa. (alama 2)

(n) **Tambua** aina za maneno katika sentensi ifuatayo:

Walicheka sana walipoambiwa hadithi hiyo. (alama 2)

(o) **Tunga** sentensi ukitumia semi zifuatazo:

(i) Kula uhondo (alama 2)

(ii) Regea parafujo za mwili (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(p) Tumia neno “mpaka” katika sentensi kueleza dhana ya:

(i) Wakati (alama 1)

(ii) Mahali (alama 1)

(iii) Kiwango (alama1)

(q) Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha pekee ‘o-ote’ katika ngeli ya u-u (alama 1)

4. **ISIMU JAMII**

Ponda mali: Karibu! Wamama wang’are mali safi ambayo huwezi kupata popote duniani.

Amina: Unauzaje hilo rinda?

Ponda mali: Bei ni kusikilizana, hatuwezi kukosana.

Amina: Nitakupaa shilling hamsini, naona ni mtumba.

Ponda mali: Mama hilo rinda ni original kutoka Marekani kwa meli.

Amina: Nitaongeza shilingi kumi basi.

Ponda mali: Ongeza kidogo, usiniue.

(a) (i) Hii ni sajili gani? (alama 1)

(ii) **Eleza** sifa za sajili uliyotaja hapo juu (alama 4)

(b) **Eleza** sifa zozote tano za sajili ya kidini. (alama 5)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA VII

KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

1(a)

- Kumdekeza mtoto (mwana) /mtoto aliyedekezwa/mtoto wa kiume/mziwanda/jinziaa.

(b)

- Walimwita mtoto hata wakati alikuwa mkubwa.
- Walimnyonyesha hadi daraasa la tano (akiwa mkubwa).
- Kumweleka Mziwanda hadi nyumbani anapotoka shuleni.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Baba kumwimbia nyimbo za kumwongoa hadi alale.
- Wazazi kumwosha hata wakati alikuwa aamevunja ungo.
- Walimpendelea zaidi ya watoto wao wengine(wa kike)

½ x6=3

(c)

- Husingizia kuwakosa wazazi wake.
- Husingizia na kulia eti chakula ni kigumu shuleni.
- Hulia eti anaona baridi shuleni Kwa vile alikuwa amezoea kulala mbavuni mwa wazazi wake.
- Akiwa na ugonjwa kama vile homa, huzingizia kuwa hatunzwi shuleni.
- Hakujua kunawa wala kuoga na alikuwa akinuka sana mbali na mavazi yake kama vile viatu.

1x4=4

(d) Semi

- Alipopigwa darabuni.
- Kupigwa msasa.
- Hamu na ghamu.
- Jitihada ziliambulia patupu.

Methali

- Mtoto akinyea kiweo hakikatwi.
- Ajabu ya shingo kukataa kulala chini.
- Mwendo kikwongonga nawe mtapike.
- Avuliwaye nguo huchutama.

Tashbihi/Tashbiha.

- Hunata kama gundi.

Tanakali ya sauti

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Naye hunuka fee!

Chuku

- Huyaacha matongo yakiwamulika watu
- Viatuni mwake ingesababisha pua kungoka na mapafu kurudi

Maswali ya mbalagha

- Utu uzima hufunzwa katika taasisi gani?
- Kwa nini wazazi wengine hawatosheki kwa kuwapata watoto wa jinsia moja tu?
-

Lakabu

- Jongoo
- Toto kuu

Kutaja ½

Mfano ½

(e)

i) Mziwanda – kifunga mimba /kitinda mimba.

ii) Kukaramuka – kukomaa.

iii) Waa – kosa

2. **Ufupisho**

(a) Binadamu alipewa.

- Uwezo wa kumiliki kila kitu.
- Akili na maarifa ya kupanga mambo yake .
- Uwezo wa kuwasiliana na wenzake kwa lugha.
- Kufaidika kutokana na mazingira yake.
- Uwezo wa kuzaa na kuijaza dunia

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

- Yeye ana uwezo wa kutumia technolojia kwa manufaa yake.
  - Ametumia nyambizi
  - Amefika mwezini.
  - Amevumbua uyoka, tarakilishi na sasa anatandaridhi.
  - Dunia yake imekuwa kitongoji

Hoja 10x ½ =alama 5.

Alama 1 ya mtiririko.

(b)

- Binadamu amekuwa dubwana linalonjenga na kubomoa.
- Viwanda vinachafua maji na kuua viumbe muhimu.
- Moshi kutoka kwa viwanda unadhuru ukanda wa ozoni na joto kuzidi duniani.
- Idadi ya binadamu imeongezeka zaidi ya uwezo wake.
- Maradhi na ufukara yamekuwa matatizo makubwa kwa binadamu
- Binadamu amefyeka misitu yote.
- Amefurusha na kuwaangamiza baadhi ya wanyama.
- Chemichemi za maji zimekauka na kuarika jangwa.

(Alama1 kwa kila hoja sahihi x 8 = 8)

(Alama 1 ya mtiririko)

Matumizi ya lugha

3(a) ✔ ✔ “Mimi naona ni kazi ngumu,” ✔ ✔ nilimjibu. ✔ ✔ “Si kazi ngumu ✔ ✔ , ni mboga tu!” ✔ ✔ ✔ Aliniambia huku akiniangalia kwa jicho la kunirai. ✔ $\frac{1}{3}$ x12=4

(b)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(i) Kikombe cha ✔ mwalimu wetu ✔ ambacho kilivunjika / ✔ kilichovunjika kilikuwa ndani ya kabati/ ✔ kilikuwa kabatini. ½ x4=2

(ii) Mgeni alikodi ✔ chumba cha kulala baada ya kuburudika kwa ✔ muziki. ½ x2=1

(c)

(i) Alitoroka kabisa. 1x1=1

(ii) Alitujia kwa mbio/alikimbia kwa niaba yetu. 1x1=1

(d) Mwalimu alimwambia mwanafunzi arejelee ✔ maelezo katika kitabu ili kuhakiki majibu yake. ✔ 1x2=2

(e)

(i) Mwanafunzi /mwalimu mlevi n.k 1x2=2

(ii) Nchi huru zaKiafrika n.k 1x2=2

(f)

- Anapenda kusoma – Fungu tenzi.
- Gazeti lenye masuala ya kijamii – fungu nomino.

1x2=2

(g)

(i) i - i

(ii) i – zi 1x2=2

(h)kitabu – yambwa. ½ x1= ½

Vizuri sana – chagizo. ½ x1= ½

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(j) Ua ambalo humea huwa limetiwa mbolea. 1x1=1

(k)

(i) Barmasai azungumza/yuazungumza kilatini vizuri. 1x1=1

(ii) Toto ✔ hili ✔ halili ✔ chakula kingi sana. 1x1=1

(l)

(i) Mhakiki/wahakiki, uhakiki, kuhakiki.

(ii) Subira ,kusubiri.

(iii)Msajili,usajili,kusajili. 1x3=3

(m)Wagonjwa ✔ wamesema ✔ wamekunywa ✔ dawa. 1x2=2

(n)walichoka sana walipombiwa hadithi hiyo.

T E T N V 1x2=2

(o)

(i) Tafrija /furahia katika burudani. 1x2=2

(ii) Kuwa na afya iliyozoroteka /mgonjwa. 1x2=2

Mtahiniwa atunge sentensi.

(p)

(i) Alicheza mpaka jioni.. n.k

(ii) Alizuru mpaka wa Kenya na Uganda .nk

(iii)Juma alitia maji mtunguni mpaka ukajaa n.k 1x3=3

(q)Mwanafunzi atunge sentensi na kivumishi **wowote** kitumike. 1x1=1

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ISIMU JAMII

4(a) Ni sajili ya sokoni /biashara.(alama 1)

Sifa

(i) Inaeleza ubora wa bidhaa.

(ii) Kuna kupiga chuku k.m huwezi kupata popote duniani.

(iii)Ina ushawishi.

(iv)Haizingatii kanuni za sarufi – wamama.

(v) Kuchanganya ndimi – original.

(vi)Hutumia lugha ya mkato.

(vii) Hujaa porojo.

(viii) Hutumia lugha nyepesi.

(b) **Sifa za sajili ya kidini.**

- Matumizi ya msamiati maalum anashauriana na dini k.m

  Ukristo: haleluya, amina, mhubiri, jehanamu, mbinguni, Yesu, mungu

  Uislamu: Allah, mtume, Alhamdullilahi n.k
- Mwelekeo mkubwa wa kunukuu vifungu kutoka vitabu vitakatifu k.v Biblia na Koran.
- Lugha inaonyesha unyonge alio nao binadamu.
- Lugha ya kunyenyekea na kutubu.
- Kuna kupanda na kushuka kwa sauti kutegemea madhumuni ya mhubiri.
- Lugha huandamana na matumizi ya ishara ili kusisitiza ujumbe.
- Maombi huenda yakasemwa kwa pamoja na waumini wote.
- Kuna sala za kujibizana – Mhubiri husema jambo kasha waumini hujibu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Mungu hupewa majina mengi ya sifa k.mMtukufu, Mwenye uwezo wote, Alfa na Omega, Rabana, Baba nk.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA VIII

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Siku hizi kuna vitambaa vya kushonea nguo aina aina na vingine vingi vinaendelea kutengenezwa. Kuna vitambaa vya pamba, hariri, vya mnato, nailoni, sufi na vinginevyo. Kadhalika kuna mitindo na rangi za kila aina.

Kutambua kitambaa cha kushonea nguo si jambo rahisi. Uchaguzi huo ni sharti ufikiriwe kwa makini sana. Mnunuzi wa vitambaa vya nguo anapaswa kufahamu kwamba kuna vitambaa tofauti tofauti vyenye sifa tofauti tofauti. Kwa mfano, baadhi ya vitambaa hukwajuka rangi na kuwa vyeupe, vingine huchanika vinaposuguliwa, vingine hurudi vikifuliwa na vingine ni teketeke au nyong'onyevu ilhali vingine hukunjana vinapofuliwa. Baadhi havipigwi pasi, na havifuliwi kwa maji baridi, vingine hufuliwa kwa maji yenye joto kiasi.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Mnunuzi anapaswa kuzingatia sifa hizi zote pale anapochagua vitambaa vya nguo. Hata hivyo, ni vizuri kufahamu kwamba sio watu wote wanaozifahamu sifa zote muhimu za vitambaa; na wale wanaozijua baadhi za sifa hizi hawazijui zote.

Kuna njia kadhaa anazoweza kutumia mnunuzi kujulia sifa za vitambaa vya nguo. Mnunuzi, kwa mfano, anaweza kuwauliza wauzaji. Ni vizuri hata hivyo, kutahadhari na kuyapima maelezo yanayotolewa kwa uangalifu. Ingawa chini ya kifungu cha sheria cha maelezo ya kibiashara wauzaji wanapaswa kutoa habari sahihi kuhusu bidhaa zao, si wote wanaosema ukweli. Hii ni kwa sababu wengine huhofia kwamba wakitoa habari sahihi huenda wakakosa wateja wa kununua bidhaa zao.

Njia nyingine ambayo kwayo mnunuzi anaweza kujulia habari za vitambaa ni kwa kuangalia maelezo yanayopatikana kwenye vibandiko au vijikaratasi vyenye maelezo. Kwa mujibu wa sheria za nchi nyingi vibandiko vya aina hiyo vinapaswa kuwa sahihi na kutoa habari zisizo sahihi ni kosa linaloweza kumfanya mtengenezaji kuadhibiwa. Maelezo yanayopatikana kwenye vibandiko hivyo ni muhimu kwa sababu hutoa maelezo muhimu kuhusu aina ya vitambaa, namna vinavyoweza kufuliwa na kama vinapaswa kupigwa pasi au la miongoni mwa mambo mengine.

Mtu anaweza kujua aina ya kitambaa pia ikiwa ana ujuzi wa kushika au " kuhisi ". Mtu anaweza kushika kitambaa kwa utaratibu na kukadiria kama kinakunjanakunjana au la. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba sio wauzaji wote ambao wanapenda vitambaa vyao vishikweshikwe kwani vikishikwa sana huishia kuwa vichafu na kukosa wanunuzi.

Baada ya uchaguzi bora wa kitambaa, uamuzi wa kama mtu fulani atanunua kitambaa kizuri au la ni bei nafuu. Ni vizuri kutafuta vitambaa vizuri na visivyo vya bei ghali. Kufanya hivyo kutamsaidia

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

mnunuzi kutotumia pesa ambazo angetumia kufanyia mambo mengine kununulia nguo tu.

Maswali

a) Toa kichwa mwafaka kwa taarifa hii. (alama 1)

b) **Mwandishi ana maana gani anaposema:** (alama 3)

i) Vitambaa vya aina aina

ii) Baadhi ya vitambaa hukwajuka au huchujuka rangi

iii) Vingine hurudi vikifuliwa

c) Taja njia tatu zilizotajwa na mwandishi zinazomsaidia mnunuzi kuchagua kitambaa bora (alama 6)

d) Taja aina nne ya vitambaa vilivyotajwa na mwandishi katika taarifa. (alama 2)

e) Je, baada ya kuchagua kitambaa unachotaka, ununuzi wa kitambaa hicho utategemea nini ? (alama 3)

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Sehemu muhimu ya elimu tamaduni ilikuwa ile ya maisha ya ndoa. Vijana wake kwa waume, kwanza walifunzwa umuhimu wa kujiheshimu kimwili kabla ya kuolewa ama kuoa. Ilikuwa mwiko na aibu kwa msichana kupata mimba nyumbani, au kwa mvulana kumtunga mimba msichana kabla ya ndoa. Kwa hivyo shida ya watoto wa haramu haikuwepo katika jamii. Mafunzo kuhusu mpango wa uzazi yalikuwa muhimu. Ilikuwa ni aibu kwa mume na mkewe kuzaa watoto kabla ya miaka miwili au zaidi kupita. Wakati wa kunyonyesha mtoto, mume na mke walitarajiwa kutoonana kimwili, na hii ilisaidia katika kumlea mtoto.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Vijana wanaume kwa wake waliaswa kuhusu kuchagua wachumba wao kwa kuelezwa ni ukoo au mbari gani ingefaa kuoa au kuolewa nao. Ndoa zote zilihitaji vibali vya wazazi wa mume na mke. Haya yalipunguza shida za talaka kwenye jamii.

Vijana walifunzwa kuyaelewa mazingira yao, hasa kuhusu hali ya anga, ili wafahamu majira ya mvua na ukame. Walifunzwa kuchunguza na kufafanua hali za miti, ndege, nyota na wanyama wengine kujua ni majira gani ya hali ya hewa wanayotarajia ili kujiandaa nayo. Mafunzo ya hali ya hewa yaliwasaidia baadaye maishani katika shughuli zao za ukulima, ili waweze kutofautisha baina ya udongo wenye rutuba na ulio dhaifu, na pia waweze kujua mimea iliyoweza kumea katika aina mbalimbali za ardhi. Kutokana na mimea ya asilia mbalimbali, walijifunza ubora wa ardhi mbalimbali katika sehemu walizolima.

Elimu tamaduni haikuacha kuwafunza vijana jinsi ya kuyakabili magonjwa kati ya jamii. Kwa hivyo vijana wengine walikulia kuwa waganga waliotegemewa na jamii yao. Matibabu ya mitishamba yalihitaji mafunzo mahususi yahusuyo kuitambua miti ifaayo kwa matibabu na matumizi katika kuponya magonjwa mbalimbali.

Elimu tamaduni ilitolewa na kufunzwa kwa dhati na watu waliofahamu mahitaji ya jamii yao vyema, kwa wakati ufaao kwa vijana wa umri mbalimbali. Mambo muhimu ni kuwa elimu tamaduni ilisadifu matakwa ya maisha ya jamii. Ilikuwa elimu ya maisha yake ya baadaye katika mazingira alimoishi.

Maswali - .

a) Eleza jinsi ukosefu wa elimu tamaduni ungeweza kuathiri jamii. (maneno 30) (alama 4)

Matayarisho

Jibu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

b) Eleza umuhimu wa elimu tamaduni katika jamii ya kale. (maneno 80) (alama 11)

Matayarisho

Jibu

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) **Unda nomino kutokana na utenzi.** (alama 1)

i) Chelewa

ii) Andika

b) **Neno 'huyu' limetumikaje (kumaanisha nini katika sentensi hizi)** (alama 2)

(i) Huyu amekuja kwangu

(ii) Mgeni huyu amekuja kwangu

c) **Tambua aina ya vishazi katika sentensi ifuatayo.** (alama 1)

Wanafunzi wanasoma darasani

d) **Tunga sentensi ukitumia kielezi cha**

(i) namna/jinsi. (alama 1)

(ii) Idadi. (alama 1)

e) **Yakinisha sentensi ifuatayo.** (alama 1)

Usipomsamehe nduguyo hutasamehewa.

f) **Kanusha sentensui ifuatayo.** (alama 1)

Mlevi alitembea kiholela halafu akaanguka chini pa!

g) **Tunga sentensi tatu zitakazoonyesha matumizi haya matatu ya 'ki'.** (alama 3)

i) Kwonyesha wakati wa masharti

ii) Kiambishi cha ngeli

iii) Kuonyesha mahali

h) **Andika katika usemi wa taarifa.** **(**Alama 3)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

"Karibu Bakari, tafadhali kaa', Juma akasema.

" Asante, Je, habari za nyumbani?" Bakari aliuliza

i) **Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.**

i) Alilala jioni. (alama 1)

ii) Mchezaji huyu ni hodari sana. (alama 1)

j) **Tumia kielelezo cha jedwali kuchanganua sentensi.** (alama 3)

Kandanda inapendwa na watu wengi sana.

k) **Andika udogo wa sentensi zifuatazo**

i) Sahani zetu ni nzuri kuliko zao. (alama 2)

ii) Njia hii inaelekea kule mlimani. (alama 2)

l) **Akifisha sentensi ifuatayo.** (alama 2)

nilimkuta mkuu wa wilaya ya fahari akisoma kitabu kiitwacho utubora mkulima.

m) **Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya vitenzi vifuatavyo katika jinsi ya kufanyiwa.** (alama 3)

i) -ja

ii) -cha

iii) -Nywa

n) **Andika methali zinazowakilisha maadili yafuatayo.** (alama 4)

(i) Mvi ni dalili ya busara

(ii) Kushika hatamu huleta adha nyingi.

o) **Andika kinyume cha;** (alama 1)

walizama walipokuwa wakikusanya mchanga

p) **Eleza maana ya misemo ifuatayo.** (alama 4)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

i) Msumari wa moto juu ya kidonda

ii) Giza la ukata

q) **Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu tofauti.** (alama 3)

Hapo ndimo alikofia

4. ISIMU JAMII

"Semeni Amen. Na ndugu atamsaliti mtoto na watoto wataondoka juu ya wazazi wao na kuwafisha. Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka".

Maswali

a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. (alama 2)

b) Fafanua sifa ya lugha iliyotumika katika mazungumzo haya. (alama 5)

c) Eleza sababu zinazofanya mazungumzo yanayotokea katika mazingira mbalimbali kuwa na sifa tofauti tofauti za kimatumizi ya lugha. (alama 3)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA VIII

KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

a) - Vitambaa mbali mbali.
- Aina mbali mbali ya vitambaa mbali mbali.
- Sifa za vitambaa mbali mbali
- Jinsi ya kununua kitambaa cha kushonea. (1 x1 =1)

b) i) – Vitambaa sampuli sampuli
- Namna mbali mbali ya vitambaa
- Aina tofauti tofauti ya vitambaa
- Sifa mbali mbali ya vitambaa. (1 x 1 = 1)

ii) – Kubadilika kutoka hali yake ya awali / kwanza (1 x 1 =1)

iii) – Kuwa fupi. (1x 1=1)

c) - Kuuliza wauzaji kwa tahadhari hasa juu ya majibu utakayopewa na muuzaji kwa vile baadhi yao waweza kudanganya au kughilibu kuhusu hali halisi ya vitambaa.
- Vijibandiko au vijikaratasi vidogo vilivyobandikwa kwenye nguo zaweza kuwa na maelezo mwafaka kuhusu sampli hiyo ya vitambaa hivyo basi mnunuzi sharti aisome na amakinike nalo kwani yaweza kuwa bandia.
- Lazima mtu awe na ujuzi wa kushika au kuhisi kitambaa chenyewe. (3x 2=6)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

d) - Vitambaa vya pamba
- `` `` Hariri
- `` `` mnato
- `` `` Nailoni
- `` `` Sufi n.k. (½ x 4 =2)

e) - Ununuzi hutegemea bei ya vitambaa vyenyewe.
- `` `` pia nyanja nyinginezo ya ununuzi na wala si nguo pekee. (2 x 1 ½ =3)

2. UFUPISHO

a) - Kupata mimba kabla ya kuolewa au mvulana kumtunga msichana mimba.
- Kuwepo kwa watoto haramu katika jamii.
- Kuzaa watoto wengi bila mpango
- Kutomlea mtoto ipasavyo. (4 x 1 = 4mks)

b) i) Vijana wake kwa waume, kwanza walifunzwa kujiheshimu kimwili kabla ya kuolewa ama kuoa .

ii) Ilisaidia katika mpango wa uzazi.

iii) Vijana wanaume kwa wake waliaswa kuhusu kuchagua wachumba wao kutoka mbari iliyofaa.

iv) Talaka zilipungua

v) Vijana walifunzwa kuchunguza mazingira yao hasa anga, miti, ndege, nyota na wanyama wengine.

vi) Iliwafunza vijana jinsi ya kuyakabili magonjwa

vii) Vijana walikulia kuwa waganga waliotegemewa.

viii) Vijana wa umri mbali mbali walifunzwa kwa wakati ufaao. (8 x 1=8)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

M a – 4

b – 8

ut – 3 (alama zote 15)

3. a) MWONGOZO : MATUMIZI YA LUGHA

i) Kuchelewa, uchelewaji, mchelewaji

ii) Kuandika, uandikaji, mwandiko, mwandishi.

b, i) kiwakilishi /Kibadala cha nomino

ii) Kivumishi

c) Wanasoma darasani

d,i) Alitembea kifahari

ii) Alikimbia mara tatu.

e) Ukimsamehe, utasamehewa

f) Hakutembea, hakuanguka.

g,i) Ukitaka kupita mtihani soma kwa bidii (Masharti)

ii) Kiti kilivunjika (KI – VI)

h) Juma aimkaribisha Bakari aketi, Bakari akashukuru na kutaka kujua habari za nyumbani.

i) i) Jioni – wakati

ii) Sana – Jinsi/ namna

j)

S					
KN		U	KT		
N	T		N	V	E
Kandanda	inapendwa	na	watu	wengi	sana

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

K,i) vijisahani vyetu ni kuliko vyao.

ii) Kijia hiki kinaelekea kule kilimani.

l) Nilimkuta Mkuu wa wilaya ya Fahari akisoma kitabu kinachoitwa "Utubora Mkulima"

m) – Jiwa

- chiwa
- Nywiwa / nywewa

n) - Jungu kuu halikosi ukoko.

- Ukubwa ni jaa

o) Walielea, wakitawanya

p) – Kuzidisha machungu / kudhuru zaidi

- Giza tororo

q) - Hapo ndipo alipofia

- Humo ndimo alimofia
- Huko ndiko alikofia.

4. ISIMU JAMII

a) Haya ni mazingira ya mahubiri. Kuna mhubiri/ kasisi na waumini/ wasikilizaji.

b) - Ni lugha ya unyenyekevu.
- Ni lugha ya kubembeleza/ kushawishi wasio waumini
- Sauti hupanda na kushuka kulingana na maudhui na pia.
- Matumizi ya msamiati maalum kwa mfano majina mbali mbali k.v Jehovah.
- Hurejelea vifungu/ sura mbali mbali katika Biblia.
- Msamiati ni wa lugha ya kikale.
- Ni lugha ya kuamrisha.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Ni lugha ya matumaini.
- Ni msamiati wastani wala si mgumu unaeleweka na mtu wa kawaida.
- Matumizi ya ishara ili kusisitiza linalosemwa/ kuwasiliana na wasiosikia.
- Kuzungumza kwa pamoja katika sala, sentensi huwa fupifupi. (5 x 1 =5)

c) - Cheo
- Umri
- Mazingira
- Elimu
- Rika (3 x 1 = 3)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA IX

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma tarifa hii kisha ujibu maswali.

Asifuye mvua imemnyea. Huu ni msemo wenye hakika isiopingika, na kutilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande magharibi badala ya mashariki.Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo, na kama halipo li njiani.Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini alishangaza umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina kirefu cha kutamauka na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mojawapo ya mafunzo ya kidini ambayo padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja wetu ni kushukuru tu. .Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

Ima fa ima, na waswahili husema, “mlaumu nunda na kuku pia”.Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kulala nje. Huenda alikosana na ndugu zake kwa kuepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia kufidia makosa yake. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na ukimwi, raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa jumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto ni adhabu inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya PN inafafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka.Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la ndoa bila haya. Huu upotofu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P..N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu huo wake.

Maswali

1. **Taja** kichwa mwafaka kwa makala haya. (alama 2)
2. Katika aya mbili za kwanza, mwandishi anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani? (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

3. **Eleza** chanzo cha tabia za P.N. (alama 2)
4. Mwandishi wa taarifa hii anataka P.N. achukuliwe hatua gani? Kwa nini? (alama 4)
5. Barua ya P.N. bila shaka imeonyesha uvumbuzi mpya. **Utaje** (alama 2)
6. **Eleza** maana ya vifungu hivi kama vilivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)
   (a) Kina kirefu cha kutamauka
   (b) Ima fa ima
   (c) Kufudia makosa yake

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii, na kwa dhati ya mioyo yetu tuweze kupata ufanisi, na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu.Tukumbuke,"Ajizi ni nyumba ya njaa ". Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja.Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu.Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbali mbali ya maendeleo.Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeke. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo pia lazima tujishugulishe na biashara ambapo kwa sasa ni wakenya wachache sasa ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wengine ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni, na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu ya kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwanakenya kujua wajibu wake katika

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

jamii. Tumesinywa na elimu pumbao inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu lazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja,"Utengano ni uvundo". Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu ,wakati tunapokosea, lazima tukubali tumekosa na kufanya masahihisho mara moja kwani, "Usipoziba ufa utajenga ukuta".Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishugulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia ya kutatua matatizo hayo siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu.Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo, lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo.Tukiwa viongozi ambao hawajishugulishi na maendeleo,basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kama kwa utajiri wake.Kwa hivyo, basi tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba kubwa au tajiri.

(a) **Eleza** dhamira ya mwandishi kwa taarifa hii (maneno 20) (alama 2)

NAKALACHAFU

NAKALA SAFI

(b) Kwa mujibu wa aya ya kwanza, mwandishi awahimiza vijana kufanya nini ili kuleta maendeleo nchini? (maneno 70) (alama 4)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

(c) Kulingana na taarifa hii ni mambo gani hasa ambayo yamechangia maendeleo kuzorota nchini Kenya? (maneno 40 - 50) (alama 6)

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

SEHEMU B

3. **MATUMIZI YA LUGHA:** **(ALAMA 40)**

(a) **Ziandike** sentensi zifuatazo ukitumia kiwakilishi cha pekee o-ote. (alama 2)

(i) Ufunguo wowote ufunguao ni wetu.

(ii) Ngozi zozote zirarukazo ni za kifaru.

(b) Taja sauti zozote nne zinazotamkiwa katika ufizi. (alama 2)

(c) **Andika** sentensi inayoonyesha 'ki' ya masharti. (alama 1)

(d) **Onyesha** viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimkemea. (alama 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(e) **Bainisha** matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Ondokeni.

(ii) Kiptoo ni mwizi sugu

(f) **Eleza** maana nne zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

(i) Alimpigia simu

(g) **Changanua** sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 3)

(i) Vile vingali vikitengenezwa

(h) **Akifisha** sentensi ifuatayo. (alama 3)

(i) puka chaka hata wewe siamini.

(i) **Eleza** tofauti kati ya sentensi hizi mbili. (alama 2)

(i) Ungesoma kwa bidii ungepasi mtihani.

(ii) Ungalisoma kwa bidii ungalipasi mtihani.

(j) **Andika** sentensi moja kwa kutumia 'licha ya'. (alama 2)

(k) Andika ukubwa na udogo wa neno rununu. (alama 1)

(i) Ukubwa ……

(ii) Udogo ……

(l) **Andika** sentensi zifuatazo kwa wingi. (alama 3)

(i) Domo limepinduliwa.

(ii) Kiwiko kimejigonga ukutani.

(iii)Ukimwi umeangamiza wengi duniani.

(m) **Unda** vivumishi kutokana na maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) Imani

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(ii) Ubora

(n) **Nyambua** vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendesha. (alama 2)

(i) – nya ……

(ii) - cha ……

(o) **Taja** maana mbili ya neno ‘mjomba’. (alama 2)

(p) **Andika** sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Ala! Huna heshima wewe mtoto!”

Mama alimkaripia bintiye

(q) **Kamilisha** methali zifuatazo. (alama 2)

(i) Ukuni juu ya uchaga .....

(ii) Simbiko haisimbuki ila .....

(r) **Eleza** maana ya misemo ifuatayo. (alama 3)

(i) Msumari wa moto juu ya kidonda.

(ii) Pasulia mbarika.

(iii)Giza la ukata.

(s) **Onyesha** kirai nomino, kirai kivumishi na kirai kielezi katika sentensi. (alama 3)

(i) Bawabu mzuri huandika ripoti ndefu mara kwa mara.

SEHEMU C

ISIMUJAMII (ALAMA 10)

Soma nakala hii kasha jibu maswali

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

"Ni ya leo mama ni ya leo.Ni ya leo baba ni ya leo. Bidii yako ndiyo bahati yako.Tishati na hamsa, shati arubaini.....Mali kutoka ng'ambo; chagua ufungiwe. Ni ya leo, ni ya leo....."

MASWALI

(a) **Taja** mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika makala haya. (alama 4)

(b) Huku ukirejelea makala, **pambanua** watumizi na mahali pa matumizi. (alama 2)

(c) **Taja** sifa za lugha inayopatikana katika sajili hii. (alama 4)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA IX
KISWAHILI 102/2

1. UFAHAMU:

1. – Mwanafunzi aliyeambukizwa ukimwi ✔
   - Ukimwi vyuoni. ✔
   - Hofu ya kuambukizwa ukimwi. ✔

   (yeyote moja) = 1x2=2

2. Kuwaambukiza wanafunzi wenzake mia moja na ishirini na wanne virusi vya ukimwi. ✔

   (1 x 2) = 2

3. Aliambukizwa ukimwi na mwanafunzi wa chu hicho ambaye alikuwa akifanya majaribio ya ualimu shuleni kwao. ✔ (1 x 2) = 2

4. – Apewe adhabu ya kifo. ✔ (1x 2) = 2
   - Atiwe nguvuni mara moja. ✔
   - Tayari amekiri kosa lake na kwa hivyo kumfanya awe na hatia. ✔

   (yoyote) (1x 2) = 2

5. Maadili hayapo tena katika vyuo vikuu nchini. ✔ (1x 2) = 2

6. – Kupoteza tumaini kabisa / kuwa katika taharuki kuu. ✔

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Daima dawamu / kwa vyovyote vile. ✔
- Kutumia watu wengine kuwatia adhabu kwa kosa lake mwenyewe. ✔

(1 x 3) = 3

2. UFUPISHO:

(a) **Hoja muhimu**:

- Kuwazindua vijanna ili wawajibikie nchi yao.
- Kuhimiza uzalendo.
- Kutimiza umuhimu wa elimu, hasa ya vijana.
- Kuchukua tahadhari ya baadaye kwani matatizo yalikuwa mengi na idadi ya watu kuongezeka.

(zozote 2 – alama 2)

(b) **Muhtasari**:

- Kuwahimiza wafanye kazi yoyote bila kuchagua.
- Kutumia elimu inayotimizia uzalendo na uwajibikaji katika jamii na kiwango cha kitaifa.

(2 x 2 = 4)

(c) **Hoja Muhimu**:

- Vijana kutafuta kuajiriwa badala ya kuwajibika kibinafsi.
- Upungufu wa kitaifa kwa watu walioelimika.
- Kutojihusisha kibiashara, kilimo.
- Kuacha uchumi wa nchi mkononi mwa wageni.
- Kukuza elimu tambuzi
- Kukosekana umoja wa kitaifa.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Kuchagua viongozi kwa misingi ya kikabila (kiukoo) pamoja na utajiri.

(Zozote 6 = alama6)

Alama 3 za mtiririko.

3. MATUMISHI YA LUGHA

(a)

(i) Wowote ufunguao ni wetu. ✔ 1

(ii) Zozote zirarukazo ni za kifaru. ✔ 1

(b) T, ✔ ½ d, ✔ ½ s, ✔ ½ z, ✔ ½ n, l, r (zozote nne)

(zozote nne) 4 x ½ = 2

(c) Nikisoma kwa bidii nitafaulu katika mtihani. ✔ 1

(d) **Alim**keme**a** ✔ ½

(e)

(i) Ondokeni – inaonyesha wingi ✔ 1– dhana ya kuamrisha.

(ii) Ni – Kitenzi kishirikishi. ✔ 1

(f) Alimpigia simu.

- Kwa niaba yake. ✔ ½
- Kuelekeza kwake ili apate ujumbe. ✔ ½
- Sababu ya kupigwa ni simu labda ✔ ½ ameiharibu.
- Simu ndicho kifaa kilichotumiwa kumpiga. ✔ ½

½ x 4 = 2

(g) Vile vingali vikitengenezwa.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

S

KN KT

W TS T ✔ 1

✔ 1 ✔ 1

Vile vingali vikitengenezwa

(h) Puka ✔ ½ chaka! ✔ ½ Hata wewe! ✔ ½ Siamini. ✔ ½ (½ x 6) = 3

(i) Sentensi ya kwanza inaeleza kuwa mhusika bado ana nafasi ya kurudia mtihani na kupita na ya pili inamaanisha kuwa mhusika ameanguka mtihani na hana nafasi ya kurudia. ✔ ✔ 2

(j) Licha ya kuimba, tulicheza mpira. ✔ 2

(k) Rununu – ukubwa – jirununu ✔ ½

- Udogo – kijirununnu. ✔ ½

= ½ x 2 = 1

(l) Wingi - Madomo yamepinduliwa ✔ 1

- Viwiko vimejigonga kutani. ✔ 1

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- Ukimwi umeangamiza wengi duniani ✔ 1

(m) Imani -Mwaminifu ✔ 1

Ubora. -Bora ✔ 1

(n) -nya - Nyesha ✔ 1

-cha - chisha ✔ 1

= 2

(o) Mjomba - Aina ya samaki ✔ 1

- Kaka au ndugu wa kiume wa mama. ✔ 1

- Mtu wa pwani au Mswahili kama waitanavyo watu wa bara. ✔ 1

(zozote mbili) = 2

(p) Mama alimkaripia bintiye kwa kukosa heshima. ✔ 2

(q) Methali:

(i) Ukuni juu ya uchaga hucheka ulio motoni ✔ 1

(ii) Simbiko haisimbuki ila kwa msukosuko. ✔ 1 = 2

(r)

(i) Msumari wa moto juu ya kidonnda – Kuharibu mambo ambayo tayari yameharibika.

(ii) Pasulia mbarika – ambia bila kuficha ✔ 1

(iii) Giza la ukate – hali ya umaskini. ✔ 1

(s) Bawabu mzuri - Kirai Nomino. ✔ 1

Mara kwa mara - Kirai kielezi. ✔ 1

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Ripoti ndefu - Kirai kivumishi. ✔ 1

SEHEMU C

ISIMUJAMII:

(a)

(i) Takriri – Ni ya leo ..... . ✔ 2

(ii) Utohozi – k.m. Tishati,shati

(iii) Inkishari (kufupisha maneno) k.m. -hamsa. ✔ 2

(2 x 2 = 4)

(b) Wachuuzi sokoni. ✔ 2

(c) – Nyimbo za kusifu bidhaa.

- Bidhaa zitatajwa.
- Lugha isiyo sanifu.
- Bei ya bidhaa hutajwa.
- Hamna maamkizi
- Matumizi ya lugha ya udokezi.

(zozote 4 x1 =4)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

KARATASI YA X

102/2(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

KISWAHILI

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafutayo kisha ujibu maswali

Limeibuka suala kwamba polisi waliokuwa wakiongoza mashtaka mahakamani sasa watakuwa chini ya himaya ya mkuu wa sheria wala si kamishina wa polisi. Ni hatua iliyo na mashiko katika utekelezaji na usimamizi wa sheria.

Hatua hiyo itasaidia kuhakikisha kwamba washtakiwa watapata haki kamili na kuzuia visa ambapo polisi wakati mwingine walikuwa wakiwasingizia washtakiwa madai ya uongo na kisha kuwatolea mashtaka.

Polisi hawapaswi kutekeleza majukumu fulani katika maongozi ya sheria kwa kuruhusiwa kuwatia nguvuni washtakiwa, kuwatayarishia mashtaka na halafu kuwafikisha mahakamani.

Maofisa husika sharti wafunzwe upya kuongoza mashtaka kuambatana na sheria, wala si kanuni za polisi wanaoongoza mashtaka, wawe mawakili waliosomea wanasheria ipasavyo sawa na mawakili hao wengine. Hali hii itazuia visa ambapo wakili huwa anafahamu sheria kuliko kiongozi wa mashtaka.

Mawakili zaidi wa umma wafaa kutengewa washtakiwa wasio na pesa za kuwalipa mawakili wa kibinafsi kuwatetea.

Hatua hizo zitaharakisha kesi zirundikanazo mahakamani na pia kupunguza idadi ya washtakiwa wanaowekwa rumande kutokana na hitilafu za kisheria.

Maswali

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

a) Yape makala anwani mwafaka Alama 1
b) Utekelezaji wa sheria mahakamani umetiwa sura mpya . Fafanua kwa mujibu wa makala. Alama 2
c) Dhihirisha kuwa washtakiwa nchini Kenya wamekuwa wakikosa haki. Alama 2
d) Shughuli za mahakama na utekelezaji sheria zahitaji kuboreshwa. Eleza. Alama 3
e) (i) Orodhesha majukumu ambayo polisi hawafai kuyatekeleza kisheria. Alama 3
(ii) Eleza sababu muhimu inayowakataza polisi kutekeleza majukumu uliyoyaorodhesha katika sehemu ya e (i) Alama 1
f) Eleza maana :- Alama 3

i) Kuwatia nguvuni
ii) himaya
iii) rumande

2. **MUHTASARI**

Soma makala haya kisha ujibu maswali

Ni dhamira ya mwanafunzi yeyote kupata matokeo mazuri katika mtihani wa kitaifa punde tu anapojiunga na shule iwe ni ya sekondari au msingi.
Matokeo hayo hutokea baada ya miaka minane katika shule za msingi na miaka minne katika shule za sekondari. Hata hivyo, punde tu matokeo yanapotangazwa, wengine hujipata wanyonge kwa kugundua kuwa wamefeli au wameambulia nunge kwa mtihani wao wa mwisho.

Miongoni mwa mambo yanayosababisha hali kama hii ni mwelekeo mbaya wa wanafunzi katika baadhi ya masomo. Tunajua kweli kuwa palipo na ushindani lazima kuwe na mshindi na mshindwa. Iwapo ungemwuliza mtahiniwa akueleze jinsi anavyohisi baada ya kushindwa kwenye mtihani wa kitaifa, hatakuwa na la ziada ila kukueleza kuwa hajaridhishwa na matokeo.
Wengine wao hata huvuka mipaka na kuyataja matokeo yao mabaya kusababishwa na vizingiti fulani au kuwakashifu walimu kwa kudai kuwa kulikuwa na hali ya kuonewa darasani. Unapochunguza zaidi, utakuta ya kuwa wanaodaiwa kuwa werevu ni walio stadi katika masomo ya sayansi yanayofikiriwa kuwa magumu.
Wakati wanaofikiriwa kuwa werevu wanapofanya vyema katika mitihani yao, wale wanaokisiwa kuwa wajinga ambao wamefeli hujipata wakiomboleza kwa huzuni kwa muda mrefu.
Swali la miaka mingi kuhusu elimu limekuwa ni kwa nini wanafunzi wote hawawezi wakafanya vyema na kufaulu katika mitihani ya kitaifa. Utafiti uliofanywa umebainisha wazi kwamba kunazo sababu kadhaa zinazochangia matokeo mabaya.
Mojawapo ya sababu hizo, na ambayo ni muhimu sana ni ukosefu wa nidhamu shuleni. Mwanafunzi wa aina hii hajali anachoambiwa na walimu na aghalabu muda wake mwingi unapotelea katika adhabu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Wakati mwanafunzi anapokosa nidhamu iwe kwa wazazi au walimu wake, masomo yake huathirika. Matokeo yake katika mitihani hayatakuwa mazuri. Ni Lazima tabia ya mwanafunzi iambatane na matokeo yake. Sababu nyingine ni mshituko unaowapata punde tu wanapoketi kwenye viti vyao kufanya mitihani ya kitaifa. Mtahiniwa anapojikuta katika hali hii, kuna uwezekano asifaulu katika masomo yake.

Kuna uwezekano wa wanafunzi aliyefeli katika mtihani wa darasa la nane kufanya vyema katika shule ya upili na kupita mtihani wake wa kidato cha nne. Ilibainika pia kuwa wale waliofaulu katika mtihani wa darasa la nane hulegeza juhudi zao masomoni na huwa hawapati alama zinazoambatana na zile walizopata katika shule za msingi.

Sababu nyingine ya kuwafanya wanafunzi kutofanya vyema katika mtihani ni kubaguliwa kwa wanafunzi hafifu na walimu na kukosa kushughulikiwa ipasavyo. Baadhi ya walimu wanapogundua kuwa wanafunzi fulani hawafanyi vyema katika masomo fulani, hawatumii muda wao mwingi kuwasukuma ili kuyaboresha matokeo. Badala yake huwashughulikia wanaoelewa haraka darasani.

Kuna wanafunzi wengine wanaochukua muda mrefu kuelewa, si ya kwamba ni wajinga, la, ni katika somo moja tu. Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha mwanafunzi kama huyu anapata nafasi ya kuelewa anachofunzwa.

Wanafunzi wengine hawafanyi vyema kwa sababu wazazi wao hawamudu kuwalipia karo kwa sababu ya umaskini, hawawezi hata kulipia masomo ya ziada kwa shule zinazosomesha wanafunzi wakati wa likizo.

Kulingana na takwimu za elimu, muda wa kawaida hautoshi kukamilisha mtaala wa masomo ya mfumo wa 8-4-4, kwani ni mpana sana. Walimu wanaombwa kushughulikia mafunzo ya ziada.

MASWALI

a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za mwanzo. Maneno (55 – 60). Alama 7

Matayarisho
Nakala safi

b) Fafanua sababu zinanzowafanya wanafunzi kutofua dafu katika masomo yao. Maneno (50 – 55) Alama 6)

Matayarisho
Nakala safi

(utiririko alama 2)

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Akifisha

Sikukuu ya madaraka nilikwenda eldama ravine kumwona yohana naye akasema atakuja kuniona pamoja na mkewe mariamu siku ya jumapili. Alama 3

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

b) **Andika katika usemi wa taarifa**
"Hivi vibanda vinatumiwa kulanguzia dawa za kulevya'', mkuu wa polisi alilalamika.
Alama 2

c) **Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo pamoja na kivumishi – ingine** **Alama 2**
i) dau
ii) Urembo

d) **Tumia mchoro wa matawi kuichanganua sentensi ifuatayo.**
Mwanafunzi mzuri ametunukiwa zawadi. (alama 3)

e) **Tumia <u>amba</u> katika sentensi hii.** Alama 1
Ua limealo huwa limetiwa mbolea.

f) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi. Alama 2
i) fisidi
ii) dhihaki

g) **Pigia mstari vielezi katika sentensi hizi kisha utambue ni vya aina gani.** Alama 4
i) Wezi walipigwa barabara
ii) Wezi walipigwa kwa bunduki

(h) **Tunga sentensi tatu tofauti zinazodhihirisha matumizi ya <u>Ka</u>.** (Alama 3)
i) Kanusha
Angelijua hasira yangu, angelifuata amri zangu. Alama 2

(j) **Tunga sentensi kwa kila mojawapo ya miundo hii.** Alama 2
i) Kishazi huru
ii) Kishazi tegemezi

k) **Sahihisha** Alama 2
i) Alikuja kunipea pesa zangu
ii) Umemwona mwenye ameenda sokoni

(l) **Tunga sentensi kutofautisha jozi hizi kimaana.** Alama 2
i) Kua
ii) Kuwa

m) **Sentensi sahili ni sentensi ya aina gani? Tunga sentensi kudhibitisha maana.** Alama 2
Maelezo .....
Sentensi

n) Andika kitenzi hiki katika kauli ya kutendeka Alama 1
La

o) **Tunga sentensi ukitumia misemo hii** Alama 2
(i) Fanya kikaka
(ii) Jia kikuku

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

p) **Tumia kiunganishi hiki katika sentensi.** Alama 1

Japo

q. **Andika udogo na ukubwa wa nomino - <u>ng'ombe</u>** Alama 2

r. **Andika visawe vya.** Alama 2

Masaibu

i) Kiwewe

s) **Tunga sentensi moja ukitumia kihusishi cha - a** Alama 1

t) **Kamilisha methali** Alama 1

Mti mkuu ukigwa

4. **ISIMU JAMII**

Mahojiani baina ya daktari na mgonjwa.

Daktari: Karibu ndani.

Mgonjwa: Ahsante.

Daktari: Unaitwa nani baba?

Mgonjwa: Naitwa Ali Makame.

Daktari: Unaishi wapi?

Mgonjwa: Ninaishi mtaa wa Majitu

Daktari: Una shida gani baba?

Mgonjwa: Mimi ninahisi baridi sana. Hata wakati ambapo jua linawaka, mimi huhisi baridi na kutetemeka.

Daktari: (Anachukua kipima joto na kukiingiza kwenye kwapa la mgonjwa) Hali hii ilianza lini?

Mgonjwa: Tangu juzi.

Daktari: Ni jambo gani linalokusumbua.

Mgonjwa: Naumwa na kifua bwana tabibu

Daktari: Je, baba unatumia sigara?

Mgonjwa: Nilikuwa nikivuta, lakini sasa nimeacha

Daktari: Unakohoa?

Mgojwa: Awali nilikuwa nikikohoa vibaya sana lakini sasa kikohozi kimepungua

Daktari: (Akiangalia kipima joto) Ala! Una joto jingi sana.

Mgonjwa: Nami huku naumia kwa baridi kali kabisa.

Daktari: Hebu tupime kifua chako (Anatoa stethoskopu shingoni na kudunga masikioni kisha anamwekea mgonjwa mgongoni). Vuta pumzi ndani! Vuta tena. Basi Toa pumzi nje. Basi kifua chako si kizuri sana. Itakubidi uchukuliwe picha ya eksirei (uyoka). Ninataka upimwe katika maabara kama una viini vinavyosababisha malaria.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Mgonjwa: Ninachotaka bwana mganga ni kupona tu.
Daktari: Utapona. Usiwe na wasi wasi (Anaita mwuguzi). Nitakudunga sindano moja ya kuteremsha hicho kiwango chako cha joto. Kisha nenda ukapewe dawa nilizokuandikia.
Mwuguzi: Nimefika daktari.
Daktari: Mchukue huyu mgonjwa umpeleke katika maabara apimwe malaria, baadaye achukuliwe picha ya eksirei.

Jibu maswali haya

a) Jadili sifa za lugha inayotumiwa. Alama 6

b) **Eleza maana ya vifaa vifuatavyo ambavyo hutumika katika mazingira ya hospitali** Alama 4

(i) Uyoka
(ii) Kipima joto
(iii) Machela
(iv) Mwuguzi

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA X

KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

a) Mabadiliko katika mahakama, sura mpya mahakamani (yoyote moja alama 1

b) Maafisa wa polisi wanaoongoza mashtaka kuwa chini ya mkuu wa sheria wala si kamishina wa polisi (alama 2 kwa maelezo)

c) (i) Polisi kuwasingizia washtakiwa madai ya uongo

(ii) Washtakiwa kukosa mawakili wa kuwatetea kutokana na ukosefu wa pesa (kila hoja alama 1 jumla (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

d) (i) Maofisa wa kuongoza mashtaka kufunzwa upya kulingana na sheria

(ii) Maofisa hao wawe mwakili waliosomea uanasheria

(iii) Mawakili zaidi wa umma watengewe washtakiwa ambao hawana uwezo wa kifedha (kila hoja alama

moja – jumla alama 3

e) (i) Kuwatia washtakiwa nguvuni

(ii) Kuwatayarishia washtakiwa mashtaka

(iii) Kuwafikisha washtakiwa mahakamani (kila hoja alama 1 jumla alama 3)

(II) Polisi hawafahamu / hawana ujuzi wa sheria jinsi walivyo mawakili (Alama 1)

(f) Kuwatia nguvuni – Kuwanasa/ kuwashika

(ii) Himaya - uangalizi

(iii) rumande – Watiwapo washukiwa
wakisubiri kutaja
au kusikizwa kwa kesi zao (ufafanuzi mzuri alama moja jumla alama 3)

2. MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

MUHTASARI

a)
- Nia ya kila mwanafunzi ni kupita mitihani
- Matokeo huwafanya wanafunzi wengine kuwa wanyonge kwa kufeli
- Wanaanguka kwa ajili ya mwelekeo mbaya wa wanafunzi katika baadhi ya masomo
- Palipo na ushindani lazima kuwe na mshindi na mshindwa
- washindwa husema hawaridhishwi na matokeo ya mtihani

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

- wengine huwalaumu walimu kuwanonea darasani
- Wanaochukuliwa kuwa werevu ni wale walio stadi katika masomo ya sayansi
- Werevu wanapofanya vyema, wajinga wanachukua muda mrefu kuomboleza

7x1=07 zozote 7 alama 7

b) Ukosefu wa nidhamu shuleni, anapoteza muda mwingi kuadhibiwa/ katika adhabu

- Wanashtuka wanapokuwa katika jumba la mitihani ya kitaifa
- wanalegeza juhudi zao masomoni hasa waliofaulu katika mtihani na darasa la nane
- walimu kuwabagua wanafunzi hafifu na kukosa kushughulikiwa
- Walimu kushughulikia wanafunzi werevu
- Wanafunzi wengine kuchukua muda mrefu kuelewa baadhi ya masomo
- Baadhi ya wazazi ni maskini hawana pesa za kulipia karo na masomo ya ziada zozote 6 x 1 =

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Sikuukuu✓ ya Madaraka✓ nilienda Eldama✓ Ravine✓ kumwona Yohana✓ naye akasema atakuja kuniona pamoja na mkewe Mariamu✓ siku ya Jumapili✓(vitahiniwa vyovyote sita x ½ = 3)

b) Mkuu wa polisi alilalamika kuwa✓ vibanda vile vilitumiwa✓ kulanguzia dawa za kulevya au: Mkuu wa polisi alilalamikia✓ vibanda vilivyotumiwa kulanguzia dawa za kulevya (kila kitahiniwa alama moja jumla alama 2)

c) Dau jingine (alama 1)

Urembo Mwingine (alama 1)

d) Mchoro wa matawi

S

(alama 1)

KN KT

N V T KN

(alama 1)

N

Mwanafunzi mzuri ametunukiwa zawadi (alama 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

e) Ua ambalo humea huwa limetiwa mbolea (alama 1)

f) Fisidi – ufisadi/ fisadi (✓ 1)

Dhihaki - Dhihaka (✓ 1)

g) (i) Barabara (✓ 1) - (Kielezi) halisi (✓ 1) (alama 2)

(ii) Kwa Bunduki - ala (✓ 1) (alama 2)

(alama moja kupigia mistari, alama moja)

(Kutambua aina – Jumla alama 4)

h) Matumizi tofauti ya ka

(i) Mtoto alifika akatusalimu, akatusemea akaondoka (mfuatano wa matukio)

(ii) Kajitazame wewe (Kuonyesha hali ya kuitoa nasaha au ushauri)

(iii) Alifanya kazi kwa juhudi nyingi, akapandishwa cheo (kuonyesha kitendo Fulani ni tokeo la kitendo cha kwanza)

(iv) Jambazi sugu akamatwa jijini katika vichwa vya habari magazetini) (sentensi zozote tatu alama 1 jumla alama 3

(i) Asingelijua hasira yangu ,asingelifuata amri zangu. alama 2

j) (i) Kishazi huru

mfano kama huu:

Otieno anasoma kitabu/ au rununu imepotea (alama 1

(ii) Kishazi tegemezi

Mfano kama huu

Jiko lililonunuliwa majuzi/ au milango iliyopakwa (alama1)

k. (i) Alikuja kunipa pesa zangu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(ii) Umemwona aliyeenda sokoni (alama)

Umemwona mwenye kuenda sokoni (alalma 1)

Sentensi zidhihirishe maana hizi

l) Kua - lelewa mahali /zidi umri/kimo

kuwa – miliki jambo/ jiingiza katika hali Fulani mf. Kuwa mlevi

m) sentensi yenye kitenzi kimoja alama 1

mama anasoma kitabu alama 1

n) Lika (✓ 1)

o) (i) Kuwa na haraka

(ii) Endea kwa fujo

p) Japo – maana ya ingawa, ijapokuwa (alama 1)

q) Ng'ombe - udogo – kijigombe

Ukubwa – Jigombe

r) Masaibu - Matatizo , maafa, msiba, shida, balaa (alama1)

Kiwewe - Kiherehere, wasiwasi, wahaka, babaiko, kizaazaa (alama 1)

s) M.f Kikombe cha Hosea

Miti ya Omar hakiki

t) mti mkuu ukigwa, wana wa ndege huyumba/ wamo mashakani (alama1)

4. **Isimu jamii (majibu)**

a) Sifa

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

1) Lugha ya ukarimu na heshima
2) Lugha sanifu
3) Lugha isiyo na matusi
4) Lugha yenye uwazi / bila kuficha ili mgonjwa apate huduma (zozote 3x2 = 6

b) (i) Uyoka - Mionzi iwezayo kupenya na kuonyesha picha cha vitu vilivyomo ndani
(ii) Kipima joto – Kifaa chenye zebaki kipimacho joto la mwili
(iii) Machela – kitanda kinachobeba wagonjwa au maiti
(iv) Mwuguzi – mtu afanyaye kazi ya kuhudumia wagonjwa (4 x 1 = 4)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM